

**NAMNA YA KUJITIBU  
UCHAWI  
NA KIJICHO KIISLAMU**

**الرُّقِيَّةُ الشَّرْعِيَّةُ**

**مِنَ السِّحْرِ وَالْعَيْنِ**

**Mwandishi;**  
**NUUHU UTHMAN (ABU NAJIIBAH)**  
**Tel. 0704 966 357/0778 512 841**  
**Email: [nuhuabunajibu@gmail.com](mailto:nuhuabunajibu@gmail.com)**

# **JEDIWALI LA YALIYOMO**

UTANGULIZI .....	4
MADHUMUNI YA KUANDIKA KITABU HIKI .....	6
MWANZO WA KUJITIBU UCHAWI KATIKA UISLAMU .....	7
ISHARA ( <i>SYMPTOMS</i> ) ZINAZOONYESHA KWAMBA UMESIBIWA NA MAJINI .....	9
ISHAARA KATIKA NDOTO ZINAZOONYESHA KWAMBA UMESHIKIWA NA MAJINI .....	10
ISHAARA ZINAZOONYESHA KWAMBA UMESHIKIWA NA MAJINI UKIWA BADO MACHO .....	11
FAIDA UNAYOPATA KWA KUJUA ISHARA HIZO .....	12
JINSI GANI MAJINI WANAMSHIKA MTU? .....	12
SIFA ZA MSOMAJI <i>RUQ'YA</i> .....	13
YANAYOKUPASA KUTEKELEZA KABLA HUJAANZA KUTIBU .....	14
DALILI ZINAZOONYESHA KWAMBA JINI AMEMPANDA MGONJWA KICHWANI .....	17
MASWALI YAKUMWULIZA JINI AKIANZA KUZUNGUMZA	18
FAIDA YA KUULIZA MASWALI HAYO .....	18
JINSI MWISLAAMU ANAVYOJIHFADHI BAADA YA KUSOMEWA <i>DUA</i> .....	20
JINSI ZA KUMSOMEA MGONJWA <i>RUQ'YA</i> .....	23
VIPI UTAMSOMEA MWISLAMU ALIYESIBIWA NA MAJINI? .....	23
KUMSOMEA MGONJWA KIPANDE CHOCHOTE KATIKA QURAN .....	26

KUTUMIA AYA ZINAZOZUNGUMZIA 'UTULIVU' KATIKA KISOMO CYA RUQ'YA .....	34
DUA UNAZOMSOMEA MGONJWA ALIYE SHIKWA NA MAJINI.....	36
DUA YA KUSOMEWA MAJINI WAKALI.....	40
TENDE NI DAWA DHIDI YA MAJINI .....	43
ASALI NI DAWA DHIDI YA MAJINI .....	44
MAJI YA 'ZAMZAM' NAYO NI DAWA DHIDI YA MAJINI .....	45
<i>HABBAT- SAUDA</i> NI DAWA DHIDI YA MAJINI .....	46
MAFUTA YA ZAITUNI NI DAWA YA MAJINI.....	47
MKUNAZI ( <i>SID'RI</i> ) NI DAWA YA MAJINI.....	48
USAIFI UNAFUKUZA MAJINI .....	49
KUJIKINGA KIJICHO .....	49
KUOGA MAJI YA MTU ALIYEKUPIGA KIJICHO NI DAWA .....	51
DUA UNAZOSOMA KUJIKINGA KUTOKANA KIJICHO.....	52
DUA ZINAZOHUSU KUJITIBU UGONJWA WOWOTE .....	56
KWA NINI ALLAH WAKATI MWINGINE HAAJIBU DUA ZA WAJA WAKE? .....	56
HITIMISHO .....	59
KUHUSU MMWANDISHI .....	60
ALIHUDHURIA SHULE ZIFUATAZO: .....	60

## UTANGULIZI

إِنَّ الْحَمْدَ لِلَّهِ الْخَمْدُ وَسَتَعْبُرُنَا وَنَسْتَغْفِرُهُ، وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنفُسِنَا وَسَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا، مَنْ يَهْدِي اللَّهَ فَلَا مُضِلٌّ لَهُ، وَمَنْ يُضْلِلُ فَلَا هَادِيَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ.

“Kwa hakika, sifa zote njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu. Tunamhimidi na tunamwomba msaada na tunamwomba atusamehe. Tunajikinga kwa Allah kutokana na ubaya wa nyoyo zetu na ubaya wa matendo yetu. Ye yote ambaye Allah amemwongoza, hakuna anayeweza kumpoteza, na ambaye amemwacha kupotea hakuna anayeweza kumwongoza. Nashuhudia (kwa roho yangu na kwa ulimi wangu) ya kwamba, hakuna kinachopawsa kuabudiwa kwa haki isipokwa Allah pekee yake, hana mshirika. Nahakikisha kwamba Muhammad (*swalla Llahu alaihi wasallama*) ni mja na Mtume wake”.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُعَاتِهِ وَلَا تَمُوْنَ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ﴾ .

(سورة آل عمران: ١٠٢)

“Enyi mliaoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife isipokua mmekwishakuwa Waislam kamili’. (*Surat A’al Im’ran: Aya 102*).

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا﴾. سورة النساء: ١

“Enyi watu! Mwogopeni Mola wenu ambaye amekuumbeeni katika nafsi (*asli*) ile ile, na akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka katika wawili hao, mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana, na (mwatazame) jamaa, hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu (anayaona kila mnayofanya)”. (*Surat An Nisaa: Aya 1*).

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا. يُصْلِحُ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَعْفُرُ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَنْ يُبْطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا﴾ سورة الأحزاب: ٧٠-٧١

“Enyi mlionamini! Mwogopeni Mwenyezi Mungu na semeni ya haki. Atakutengenezeeni vizuri vitendo vyenu, na atakusameheni madhambi yenu; na anayemtii Mwenyezi Mungu na mtume wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa” . (*Surat Al- Ah'zaab: Aya 70-71*).

**Baada ya hayo:**

أَمَّا بَعْدُ: فِإِنَّ حَيْرَ الْحَدِيثِ كِتَابُ اللَّهِ، وَحَيْرَ الْهَدْيِ هَدْيُ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، وَشَرَّ الْأُمُورِ مُحْدَثَّاهَا، وَكُلُّ مُحْدَثَّةٍ بِدُعَةٍ، وَكُلُّ بِدُعَةٍ ضَلَالَةٌ، وَكُلُّ ضَلَالَةٍ فِي النَّارِ.

"Maneno yanayozidi kwa ukweli, ni kitabu cha Allah. Uongozi Una ozidi kwa uzuri, ni uongozi wa Muhammad (*swalla Llaahu alaihi wasallama*), vitu ambavyo vinazidi kwa ubaya, ni vya kubuni (katika dini), kila kinacho buniwa ni uzushi, na kila uzushi ni upotevu, na kila upotevu ni wa motoni".

(Ndugu msomaji, maneno hayo ambayo nimetafsiri kwa Kiswahili, tena nikaya fanya kuwa utangulizi wa kitabu hiki, ndiyo maneno ambayo Mtume Muhammad (*swalla Llaahu alaihi wasallama*) aliyokuwa akitanguliza akiwa anaanza kukhutubu, walakini hayatumiki katika ufungishaji wa ndoa peke yake).

## MADHUMUNI YA KUANDIKA KITABU HIKI

Katika kitabu changu nilichoandika kuhusu '*Majini na Mizimu Katika Uislamu*', nilionyesha kuwepo kwa viumbwe hao, tena ni-kaandika sababu zaidi ya *sitini* (60), zote zikiwa zinahusu viumbwe hao.

Kitabu hiki kinahusu kujitibu uchawi katika Uislamu. Pia, kinahusu kutibu kijicho na magonjwa ya namna nyingine. Nilipokua naandika kuhusu majini, niliona kuwa ni muhimu sana kuonyesha yale Muislaam anayopasa kujua kabla hajatibu uchawi, baada ya kushambuliwa na viumbwe hao ambao hawapendi kujidhihirisha wazi mbele ya watu.

Kama ilivyo katika vitabu vyangu vyote nilivyovitunga, na hiki nimekiandika katika misingi miwili; Qur'an takatifu, na Hadith sahihi za Mtume Muhammad (*swalla Llahu alaihi wasallama*). Pamoja na haya, katika kuzidisha ushahidi, nimeshudisha maneno ya wajuzi katika Uislamu mbayo nimeona kwamba yanambatana na asili mbili hizo.

Ilikua huruma nyingi kutoka kwa Allah alietukuka, alipotuonyesha na kutufundisha jinsi ya kutibu uchawi, husuda na kijicho. Kwa kuwa majini ni mfano wa hewa, tusingweza kupigana nao kwa kutumia fimbo pamoja na makofi, isipokuwa Allah ametufundisha maneno ya kutusaidia.

Maneno hayo, ndio kila Muislamu anapaswa kuzingatia; sio kwenda kwa waganga wa kienyeji, wapigaji ramli ama kuombewa na mtu asiyekuwa Muislamu.

### **MWANZO WA KUJITIBU UCHAWI KATIKA UISLAMU**

Kutoka zamani, Manabii wa Mwenyezi Mungu walikuwa wanawatibu waja wa Allah wenye kusibiwa na majini kwa njia za Kisheria. Hata Wafuasi wao walifanya kazi hiyo wakishikamana na mafundisho ya Manabii wao.

Hapa Uganda, tiba ya uchawi ilianza kwa **kutumia waganga wa jadi**. Tiba hii, ilikuwepo katika kila sehemu, na mionganii mwa tamaduni ni za hapa Uganda. Waganga wa kienyeji walikua wakipiganisha majini katika madhehebu ya waganga wa jadi, bila kumhusisha Mwenyezi Mungu.

Aina nyingine ya pili, ilikua ya **kupiga ramli**. Aina hiyo ilikuwa haina tofauti na ya kwanza ya kuganguliwa, kwa sababu yenyewe ilikuwa ya kupiganisha majini, wale wanaozidi wenzawo nguvu ndio waliokuwa washindi. Wenye kufanya haya, walijifanya Waislamu kwa kutumia kitabu cha Quran. Hii, iliwaapelekea watu wengi kufikiria kuwa Quran ni kitabu cha wachawi, **wal iyaadhu bi-Llaahi**.

Aina nyingine ya kujitibu uchawi ilikua katika makanisa ya wanaoyita waokovu (*born-again Christians*). Katika kitabu changu '*Vinavyompasa Muislamu kujua kabla hajasomewa Ruq'ya*' tuliona *Fat'wa* ya wajuzi kutoka Saudia inayokataza Waislamu kuombewa makanisani. Katika dini ya Uislamu, Allah peke yake ndiye anastahili kuabudiwa na kuombwa akuponye ugonjwa wa uchawi na kuondolewa misiba na shida. Mwenyezi Mungu (Allah) indiye anastahili kuabudiwa, siyo kwenda kwa mtu mwingine asiekuwa Muislamu ambaye haamini Mungu Mmoja akuombee.

Katika mwaka **1990** hapa Uganda, Mashekhe wetu walianza kufundisha Waislamu aina ya matibabu mazuri kuhusu uchawi katika Quran na Hadith za Mtume Muhammad (*swalla Llahu alaihi wasallama*). Walionyesha Waislamu ubaya wa kujitibu kwa kupiganisha majini, kupiga ramli na kuombewa na mtu ambaye sio Muislamu. Mmoja wapo ni marehemu **SHEIKH ABDUL KARIM ABDU NUUR SENTAMU** katika Masheikhe wetu hao.

Namuomba Allah Mwenye rehema nyingi amlipe thawabu kubwa, na amlipe kila ye yote aliquosiriki katika mambo haya, kwa sababu na mimi singeweza kutunga kitabu kama hiki bila ya usaidizi wao.

Mafundisho hayo, yalienea sana katika nyoyo za Waislamu, na walishuhudia kwa macho yao jinsi ya kujitibu kwa Quran pamoja na Dua za Mtume Muhammad (*swalla Llaahu alaihi wasallama*), na Allah akawajibu kwa njia za ajabu.

Namwomba Mwenyezi Mungu anisamehe yale ambayo naweza kuteleza kama binadamu katika kitabu hiki, tena namwomba akifanye kuwa cha maana sana kwa hao wanaokisoma pamoja ha Dua ambazo nimeweka katika kitabu hiki, na zingine ambazo sikuandika.

### **ISHARA (SYMPTOMS) ZINAZOONYESHA KWAMBA UMESIBIWA NA MAJINI**

Katika kitabu chake '*Al-Wigaayah, ukraasa 67-69*', Mheshimiwa **Shk. Abdu Salaam Waheed Baali** kutoka Misiri, mwenye ujuzi katika viumbe wa kijini, alipokuwa anaonyesha ishara hizo, alisema hivi kwa ufupi:

*"Ugonjwa wa kushambuliwa na majini, hufanana na ugonjwa wa kawaida unaoathiri mwili. Kuna ishara zinazo kuwa tafauti na ishara za ugonjwa huo wa kawaida. Pamoja na hayo, ugonjwa huo kuna kipindi unapoteza ishara kufanana na ugonjwa mwingine unaoathiri mwili. Kwa mfano. siku moja kuna mwanamke mgonjwa alikuja kwangu nikamwuliza kinachomwuma. Kwa kunijibu aliniambia eti anaumwa miguu. Nikamwambia kwamba kupata uhakika, nafaa nikusomee Quran. Nilipomsomea, jinni alimpanda kichwani akasema kwamba alikuwa amemkalia miguuni. Nikamwaamuru kwamba amtoke kwa kumcha Mwenyezi Mungu, akamtoka. Mwana mke huyo akatembea bila kusikia maumivu yoyote. Allah ndiye mwenye mazuri yeye pekee".*

## **ISHAARA KATIKA NDOTO ZINAZOONYESHA KWAMBA UMESHIKIWA NA MAJINI**

Kujua ishaara hizo ni muhimu sana kwa upande wa tabibu (msomaji Ruq'ya), na Ishara hizo niza aina mbili:

- 1. Kuna zinazoonekana katika ndoto, na**
- 2. Kuna zinazoonekana ukiwa macho.**

Moja ya ishara zinazoonyesha kwamba umeshikwa na majini katika ndoto, *Shk. Abdu Salaam* alizungumzia ishaara kumi na mbili, na ndizo hizi hapa chini:

1. Mtu kushindwa kupata usingizi muda mrefu bila sababu inayoeleweka.
2. Kushtukashtuka katika usingizi kupita kiasi.
3. Kuona kitu kinachokutisha ukataka kupiga kelele (nduru) lakini sauti ikashindwa kutoka.
4. Ndoto za maajabu (*nightmares*).
5. Kuona wanyama katika ndoto kama paka, mbwa, farasi, nyoka, simba, mbwa-mwitu au panya na kadhalika.
6. Kutafuna meno ukiwa omelala.
7. Kuamuka ukatembea ukiwa kwenye usingizi bila kujifahamu (*sleep walking*).
8. Kuota unaanguka kutoka sehemu ya juu sana.
9. Kuona katika ndoto kwamba uko kwenye kaburi.
10. Kucheka, kulia au kupiga kelele katika usingizi.
11. Kuona watu ambao sio wa kawaida, kama mtu mrefu sana, mfupi sana au mweusi sana.
12. Kuona vitu halafu vikapotea. (Soma kitabu chake '*Al-Wiqaayah*'.

Hizo ndizo ishaara za kwanza kuonekana Allah akiwa ana kuonyesha kwamba upo kwa hali ya hatari ya majini yanayokushambulia. Hayo unayokuwa unaona katika ndoto, unafaa uelewe kwamba, ni majini wanaokusumbua. Maana yake, majini wakikuonyesha vitu hivyo, wanakuwa wanakutia hofu moyoni mwako kusudi waweze kukushika na kukukabili. Majini wanaharakisha sana kumdhuru mtu anapokuwa mwenye hofu nyingi sana.

**ISHAARA ZINAZOONYESHA KWAMBA  
UMESHIKIWA NA MAJINI UKIWA BADO MACHO**

**Shk. Abdu-Ssalaam Waheed Baali** alipomaliza kuleta ishara zinazoonekana kwa mtu akiwa amelala, aliongeza akaonyesha ishaara zinazoonekana kwa mtu akiwa bado macho kama zilivyo hapa chini:

1. Kuumwa kichwa kila mara pasipo na ugonjwa wa macho, shingo au tumboni.
2. Kuchukia mambo ya dini, kama kuswali ama kumkumbuka Mwenyezi Mungu (*dhikri*).
3. Kuwa mahali lakini ukawa kama haupo.
4. Uvivu mwangi mwilini pamoja na uchovu kupita kiasi.
5. Mishipa ya miguu kufangazi.
6. Maumivu katika viungo vya mwili yalioshinda madaktari kuyatibu.

Hizo ndizo ishara zinazoonekana ukiwa macho. Unapokuwa katika hali hii, unapasa kufanya wanayofanya watu wenye kushambuliwa na majini kama tutakavyoona hapo mbeleni.

## **FAIDA UNAYOPATA KWA KUJUA ISHARA HIZO**

Watu wengi wanashambuliwa na majini, lakini kwa kutoelewa ishara hizo, majini yanaendelea kuwadhuru na wakati mwengine wanapoteza maisha yao. Wengine kutoelewa ishara hizo, wanaendelea kufikiria kuwa ni ugonjwa wa muhemuko '**stress**' au ugonjwa wa mwilini. Ukielewa ishaara hizo, unafanikiwa sana.

Kwa kufikiria kuwa ni ugonjwa wa muhemuko '**stress**', baadhi ya watu wanawakimbilia waganga wa jadi ambao hawawezi kuwasaidia. Wakati mwengine, wanakimbilia kwa madaktari wanaotibu ugonjwa wa mwili, na huko hawawezi kupata msaada wowote.

Ugonjwa wa majini (**uchawi**), kwa muda mwangi, hauwezi kutibwa na dawa ambayo inatibu ugonjwa wa mwili, kwa sababu hiyo, mtu kama ameelewa ishaara hizo anakuwa amejua sehemu anayofaa kwenda, asifanane na mtu ambaye amechukua mgonjwa wake kwa **makanika** wa gari.

Mwana mke huyo tulietaja kisa chake hapo juu, angelijua kwamba ni majini waliomshambulia, asingepoteza muda akienda kwa madaktari wa kisasa.

## **JINSI GANI MAJINI WANAMSHIKA MTU?**

Majini yana aina nyingi yanavyomwingia, na hizo aina, ndizo hizi hapa chini:

1. Kuna kipindi yanamshika mtu kwenye mwili mzima, kama kutoka kwenye kichwa na hadi miguni.
2. Kuna kipindi yanashika kiungo kimoja, kama mkono, mguu au katika ulimi.

3. Kuna kipindi yanakushika muda mrefu, wakati mwingine siku mzima, au katika maisha yako yote ukawa mwedu (mwenda wazimu).
4. Tena kuna wakati yanakushikwa mda mfupi ambao haufiki hata dakika, kama kubanwa katika ndoto.

### **SIFA ZA MSOMAJI *RUQ'YA***

Kutibu mgonjwa kwa kutumia Quran au Dua, ni kazi za kitaalamu zisizofanywa na kila mtu. Anayefanya kazi hiyo, anapaswa awe na sifa zifuatazo, nazo ni:

1. Anafaa kuamini kwake na kuelewa kwake Uislamu kuwe kunaambatana na hao waliotangulia kama Maswahaba, na hao waliowafuata.
2. Anapasa kuwa ana uhakika kwamba Quran na Dua za Mtume Muhammad (*swalla Llahu alahi wasallama*) zina dhuru na kufukuza majini washambulizi.
3. Anapaswa kuwa hamshirikishi Allah aliyetukuka na kitu cho chote.
4. Anapaswa kuwa anafahamu hali za majini na vitimbi vyao.
5. Anapasa kuwa anajua ujanja wa majini na jinsi yanavyotelezesa watu. Kwa mfano, siku moja Shk. Ibn Taymiyyah (661-728 HJ) kwa kutaka kumtelezesha, jini alimwambia '**namtoka mtu huyu kwa ajili yako**', Sheikh akasema '**mtoke kwa ajili yakumtii Allah na Mtume wake**'. Angelimwambia kwamba '**mtoke kwa ajili yangu**', (Sheikh) angelikua ameteleza tayari.
6. Inakuwa bora kama anayemsomea mgonjwa *Ruq'ya* awe ni mtu aliyeoa. Mtu ambaye ameoa, anakuwa na ulinzi mkali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kutokana na kufitinika na wanawake.

7. Anapaswa kuwa anafanya *dhikiri* za kulala, za kuamka, za subuhi na jioni na zingine ambazo hazina wakati mahsusisi.
8. Kwa kutibu unapaswa kuwa unamhusisha sana Allah kwa kila jambo na ukahakikisha kwamba ndiye anayeponya; hana kinachomshinda.

## YANAYOKUPASA KUTEKELEZA KABLA HUJAANZA KUTIBU

Kabla hujaanza kumsomea mgonjwa *ruq'ya*, kuna vitu vinavyopaswa kwanza kutayarisha vizuri. Vitu hivyo, vinahusika na mahali ambapo unamtibia mgonjwa. Wakati mwingine vinahusiana na mgonjwa ambaye umeenda kumsomea. Navyo ndivyo hivi hapa chini:

1. Kuzitoa picha zote eneo ambalo unamsomea mgonjwa *Ruq'ya* kwa sababu malaika hawaingii sehemu ambayo kuna picha za viumbe ambavyo vyenye nyoyo.
2. Kuhakikisha mgonjwa amezitoa hirizi, matalasimu na vingine kama hivyo akiwa anavyo.
3. Sehemu hiyo isiwe na mtu ambaye anamchukiza Mwenyezi Mungu. Mfano kuwa na mwanaume mwenye kuvali kitu ambacho hakikubaliwi kisheria, mfano kama dhahabu au kuvali mikufu ya kike.
4. Kwanza kumfundisha mgonjwa somo ambalo linahusu kumcha Mwenyezi Mungu na kumpwekesha peke yake, kusudi moyo wake wote umwelekee Allah kwa kumtegemea amponye.
5. Sehemu hiyo isiwe na nyimbo, msalaba au kengele ambazo zinalia.

6. Matibabu yako yawe tofauti na ya wale wasiotibu kisheria, kama wale **wanaopiga ramli**, waganga wa jadi ama wale wenye kumshirikisha Allah.
7. Mfafanulie mgonjwa kwamba, Qur'an na Dua unazomsomea, sio zinazotibu bali ni Mwenyezi Mungu.
8. Umwonyeshe mgonjwa kwamba wewe unatibu, kisha Allah anaponya.
9. Kwanza unapaswa kutawadha, na kumwambia mgonjwa kupata udhu na hata wale waliopo sehemu hiyo.
10. Mgonjwa kama ni mwanamke usimsomee kabla hajajifunika kisheria, asije akaonyesha uchi wake. Akiwa mwana ume, hafai kuva suruali fupi, kuonyesha kitovu au kuva mavazi yoyote ambayo hayakubaliwi katika Uislamu.
11. Umwombe sana Allah aliyetutuka kwa nguvu zake akusaidie kumtowa jini katika mwili wa mtu huyo. Usitake watu wakuone kama mtu hodari au shujaal!
12. Usimtibu mwanamke pasipokuwa na maharimu wake.
13. Usikubali kuwepo watu wasio maharimu wake, labda kama ni hali ya dharura.
14. Usimsomee mgonjwa na niya ya kuwa jini ampande kichwani. Msomee kwa niya ya kumfukuza, kwa sababu mgonjwa huwa kwenye dhiki sana. Mtume Muhammad (*swalla Llahu alaihi wasallama*) alitahadharisha kutamani kukutana na adui wetu.
15. Allah kama amefanya maajabu jini akaongea, usikubali kila jambo analokwambia, kwa sababu ni waongo sana.
16. Usichukue mda mrefu ukimwuliza mgonjwa hiki na kile, kwa sababu jini atakamtoka, anabaki anaumia sana kicwani.
17. Allah akikuwezesha akakimbia, usibaki unajigamba kwamba umemfukuza; sema kwamba Mwenyezi Mungu ndiye amemtoa.

18. Akiwa amemtoka, kwanza msujudie Allah, kwa sababu unapaswa kumshukuru Allah kwa uwezo ambao amekujalia kumfukuza adui huyo ambaye haonekani. Ni bora mgonjwa afanye hivyo na wengine wote wanaokuwepo.
19. Usikubali masharti ya jini kwamba ataenda kwa sharti kadha. Mfano kukuomba kumchinjia kuku, kumpa dhahabu n.k ili atoke.
20. Labda kama anakwambia kwamba ataenda lakini mgonjwa huyu awe anaswali,hivyo sio vibaya. Lakini mgonjwa anapasa kuswali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu pekee.
21. Kama jini atakutukana au akakwambia kauli yenyе kuchukiza uskasirike, jini hutaka sana ukasirike ili apate nafasi ya kukuwingia.
22. Akikuogopesha, na wakati mwingine akakwambia kwamba anaenda kumwua mgonjwa wako, au wewe mwenyewe,au mmoja katika watu wako, usiogope kwa sababu Allah alisema katika Quran tukufu:

.....إِنَّ كَيْدَ الشَّيْطَانِ كَانَ ضَعِيفًا ﴿٧٦﴾ . (سورة النساء: آية ٧٦ )

### **Maana yake:**

“.....*hakika hila za shetani ni dhaifu* ”. Soma (*Surat An-Nisaai: Aya 76*).

23. Unaweza kumsomea Aya hiyo, ahakikishe kwamba unafahamu udhaifu wake tena kwamba haujaogopa vitisho vyake.
24. Mwulize mtibiwa akweleze namna ya watu anaowaota katika ndoto.Hiyo inakusaidia kuelewa vizuri dini ya jini ili uelewe jinsi ya cha kumweleza kama atongea.Kwa mfano, anaweza kukwambia kuwa anaona watu ambao wamevaa kama Waislamu au kama watu wa dini nyingine.Majini katika ndoto, wanapenda sana

kujishabihisha (kujifananisha)na dini ya yule ambaye amewatuma.

**25.** Mwulize maswali ili yakusaidie kuelewa kama unaomwathiri ni uchawi.

### **Kwa mfano unaweza kumwuliza hivi:**

- a. Kuna wanyama ambao unawaona kwa ndoto?
- b. Wako wa ngapi?
- c. Unapowaona wanakuwa aina moja?
- d. Huwa wanakufukuza au kukuogopesha ?
- e. Kuna kipindi unaota kama unaanguka kutoka sehemu ya juu?
- f. Kuna kipindi unaota ukiwa unatembea katika wafu au sehemu ambapo hakuna watu ?

Maswali kama hayo unamwuliza mugonjwa kusudi uhakikishe kwamba kinacho muuma ni ugonjwa wa kushambuliwa na majini (**uchawi**).

### **DALILI ZINAZOONYESHA KWAMBA JINI AMEMPANDA MGONJWA KICHWANI**

Mtu mwenye kuingiliwa na majini, pindi aamuapo kumwendea tabibu wa kisheria, jini huondoka kichwani mwa mgonjwa, lakini huyu jini maadamu yuko kwenye mwili wa mgonjwa, huwa hawezি kuvumilia maumivu kutokana na kisomo. Hapo ghafla huyu jini hupanda na kwanza kujieleza.

Kuhakikisha kwamba wamempanda mgonjwa kichwani, utaziona baadhi ya dalili hizi hapa chini:

1. Kufumba macho au kuyakodoa kwa sana.

2. Kupepesa pepesa macho.
3. Mgonjwa kuyashika macho.
4. Kutetemeka mwili mzima au kiungo kimoja.
5. Kupiga kelele sana.
6. Kukwambia jina lake, kwa mfano mimi ni '**Darawesh**' au '**Namuzinda**'. Wakati mwingine, majini wanapenda sana kujiita majina ya mizimu ambayo inaogopewa sana na watu.

### **MASWALI YAKUMWULIZA JINI AKIANZA KUZUNGUMZA**

Jini aanzapo kuongea kupitia kinywa cha mtu ambaye unamzingua,inatakiwa umwulize maswali yanayo ambatana na hali hiyo.Sio kumwulizi maswali ambayo hayahusianana shuguli hiyo. Haya chini ndiyo baadhi ya maswali unayouliza:

- a. Jina lako ni nani? (Kama bado haja kwambia).
- b. Ni ipi dini yako?
- c. Kitugani kilichokufanya kuja kumshambulia mtu huyo?
- d. Uko peke yako au mko wengi?
- e. Kuna ambaye amekutuma?
- f. Kuna uchawi ambao umemfanyia mgonjwa?
- g. Katika mwili, unakaa sehemu gani, n.k?

Pamoja na hayo, kuna kipindi unasimamisha acha kuuliza majini swali lolote ukawaamuru watoke kwenye mwili wa mgonjwa.

### **FAIDA YA KUULIZA MASWALI HAYO**

Jini iwapo atakuwa mkweli katika kuyajibu maswali, unakuwa umesaidika kama ilivyo hapa chini:

- 1) Akikueleza jina tofauti nalile la mgonjwa, hapo unaelewa amempanda mgonjwa kichwani, kwa sababu mgonjwa anakuwa anajua majina yake.
- 2) Kuelewa dini yake, unakuwa umepata jinsi utakavyomwuliza.

Mfano, jini akikwambia kwamba yeze ni '**Mwislamu**', mwonyeshe kwamba Uislamu unakataza kuhangaisha viumbe wengine. Akikwambia kuwa yeze sio Mwislamu, jaribu kumfahamsha Uislamu. Akisilimu, Allah alietukuka atakulipa thawabu nyingi sana. Lakini akikataa, usimlazimishe, kwa sababu kuwa Mwislamu ni hiyari.

Kwa kujua kilichosababisha kuvamiwa, inakusaidia kwa njia ifuatayo:

- I. Kama jini ametumia fujo kwa kumshambulia mgonjwa, utamwonyesha ubaya wa kitendo hicho ili aweze kumwacha mugonjwa.
- II. Lakini mgonjwa akiwa kama ndiye sababu ya kushambuliwa na majini, inakusaidia kumwelezea kama amemaliza kumtoka, na kuonyesha majini kwamba, walichokifanya kumshambulia mgonjwa huyo siyo vyema.
- III. Kwa kuelewa wingi wao, inakusaidia kwa aina nyingi. Moja wapo ni kuwa, wakiwa wapo wengi mwilinii, na anayeongea ni mmoja, hata kama ameondoka, haimanishi kwamba shida inakuwa imeisha.
- IV. Kwa kufahamu mtu aliyemtuma, kuna kipindi unamweleza waziwazi akafahamu kwamba umemgundua. Akijua umemfahamu, wakati mwingine

mchawi huyo anaamua kuwaamuru wamtoke mgonjwa huyu. (**Katika mwaka 2004, kuna mtu alidhaniwa kuwa amewatumia majini kwa Mwislamu wamuwe, lakini mimi mwenyewe nilipomtumia Shiekhe wetu, marehemu Abdul-Hakim Sekimpi akaamwelezea wazi, Mwislamu hakurudia kupata mashambulizi yoyote**).

- V. Kwa kumjua mchawi, akiwa katika nchi ambazo zinahukumu kwa *Sharia* za Uislamu, mchawi huyu anakatwa shingo.
- VI. Kuelewa sehemu ya mwili ambapo wanakaa, inakusaidia kupakamata au kupashika wakati unamsomea Dua, kwa sababu Mtume Muhammad (*swallah Llaahu alaihi wasallama*) ndivyo alifundisha.

### **JINSI MWISLAAMU ANAVYOJIHIFADHI BAADA YA KUSOMEWA DUA**

Wakati mwingine majini wakipanda mtu, kuna sehemu wanapitia. Sehemu hiyo inapaswa kuzibwa baada ya kumsomea mgonjwa Dua.

**Mfano:** Kama mwizi anaiba sehemu, akiwa amepitia mlangoni ambao haukufungwa, na mkamfukuza akiwa ameiba au hakuiba, haiwi vyema tena kesho kuuwacha mlango huo wazi.

Hali kadhalika, ukimaliza kumsomea mgonjwa *Dua*, mpe '*dawa*' hii iliopo hapa chini:

1. Mwusie ajitahidi kusaali Swala za jamaa, kwa sababu shetani anaharakisha kumwingia na kumshawishi mtu asiyе swali Swala za jamaa.

2. Kutosikiliza mziki popote unapokuwa unachezwa, kwa sababu sehemu ambayo kuna mziki, shetani wanakuwa wengi. Ndio maana waganga wa jadi huita mizimu na majini wao kwa kuimba.
3. Kwanza tawadha kabla hujalala iwe mchana au usiku.
4. Soma sana *Suurat Al-Baqara* yote nyumbani, kwa sababu shetani hawaiingii katika sehemu inayosomwa Sura hiyo. (**Kama hawezi kusoma, ni bora asikilize kupitia mkanda hali ya kuwa anafanya bidii kujua kuisoma**).
5. Kusoma Aya mbili za mwisho katika *Surat Al-Baqara* kabla hujalala.
6. Kusoma *Ayat al- Kur'si- 255, Surat Al-Baqara*) kabla hujalala.
7. Kusoma Dua za kulala na zakuamuka. (**Soma kitabu cha marehemu Shk.Abdul Karim Sentamukilichokusanya baadhi ya Dua hizo**).
8. Soma Dua za asubuhi na za jioni kila siku. (**Soma kitabu cha marehemu Shk. Abbas Ayyub Kirevu**).
9. Soma *dhikiri* hi hapa chini kila siku mara mia moja (100) na kuzidi: '*Laa ilaaha illa-Llaahu wa'hdahu laa shariika lahu, lahul mul'ku, wa lahul ham'du, wa huwa alaa kulli shayin Qadiir*'.
10. Soma sana Quran kila siku na kuisikiliza.
11. Soma sana *Dua* au *dhikiri* ambazo zina muda maaluum, mfano kama za kutoka nyumbani na nyingine ambazo ha zina muda maaluum na sehemu.
12. Kuwa na marafiki wanaomcha Mwenyezi Mungu. Watu wanaomwuogopa Allah sana wanakuwa na Malaika wa kuwalinda . Ukihusiana nao, unakuwa umeepukana na sheitani.
13. Kusoma '***Bismi-Llah***' kila unapokuwa unaenda kufanya kitu kama kunyanyuka, kukaa, kuweka kitu

chini na vinginevyo. Lakini pakiwa na *dhikirimaalum* kwa kitu ambacho unaenda kukifanya, unasoma kama ilivyo.

14. Kunywa na kuoga maji ya *Ruq'ya* na pia kunyunyiza kila sehemu na pembe ya nyumba. (Ushahidi wa maji ya *Ruq'ya*, soma kitabu changu '*Vinavyompasa Mwislamu kujua kabla hajasomewa Ruq'ya*'.
15. Kunywa maji ya 'zamzam', na niya Allah akuponye kutokana na matatizo ya majini.
16. Kula tende saba (7), sana sana za huko Madina pindi unamkapo asubuhi.
17. Kunywa au kutafuna *habbat –saudaa*.
18. Kunywa mafuta ya mti wa 'zaituni' au kujipaka.
19. Kunywa na kuoga maji ya mvua.
20. Kuyatwanga majani ya mkunazi (*sidiri*), kisha kuyachanganya na maji na kuyaoga.
21. Kunywa asali safi ya nyuki, na usichanganye na maji ila kwa maelekezo ya tabibu.
22. Kujihifadhi katika usafi wa mwili wako; mavazi yako na mahali unapokaa.

Sababu hizo nilizozitaja, humsaidia sana mgonjwa kutoshambuliwa tena, na hata akishambuliwa majini hawawezi kumdhuru in-sha-Allah. Kila Mwislamu anapaswa kujihifadhi vizuri hata kama haujavamiwa na majini. Ukijikinga kwa namna hii, Allah hukulipa thawabu nyingi, na hapo shetanihupata uzito kuja kukushambulia. Sababu tisa za mwisho, kuanzia kwa ya kumi na tano (15) hadi kufika kwa ya ishirini na tatu(23), ushahidi utaupata mbeleni katika kitabu hiki *in-sha-Allah*.

## **JINSI ZA KUMSOMEA MGONJWA *RUQ'YA***

Jinsi zakumsomea mgonjwa *ruq'ya* ambazo nimezihakikisha ndio hizi hapa chini:

1. Kumsomea mgonjwa ukiwa unamnyunyizia maji ya *ruq'ya* sehemu ambayo inamwuma.
2. Kumsomea ukiwa unapuliza sehemu ambayo inauma.
3. Kumsomea bila kumpuliza.
4. Kutema mate kwenye mchanga, na kumsomea kisha kupaka jipu ambalo linauma.
5. Kusoma ukiwa umeshika sehemu anayoumwa mgonjwa, au wewe mwenyewe panapokuwa panakuuma.
6. Kusoma ukiwa unapanguza sehemu inayomuuma mgonjwa.
7. Kusoma ukiwa unamnyunyizia mgonjwa maji ya *Ruq'ya* katika mwili wake wote.
8. Kumsomea mgonjwa kwa sikio lake.

Hii ya mwisho siri yake ni kwamba maneno hayo yanaingia vizuri kwa mwili ambao kuna adui. Lakini piya usipomsomea kwenye maskio, tiba inapatikana kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

## **VIPI UTAMSONEWA MWISLAMU ALIYESIBIWA NA MAJINI?**

Kwa kumsomea Mwislamu aliyesikwa na majini, tumia Quran takatifu au Dua za *Mtume* (*swall Llaaha alaihi wasallama*) alizo kuwa akizitumia. Kadhalika hamna ubaya kutumia Dua au maneno yako binafsi, lakini kutumia Quran na Dua za Mtume Muhammad (*swalla Llaaha alaihi wasallama*) ndio bora.

Anza kwa kuweka mkono wako wa kulia juu ya sehemu inayouma au juu ya kichwa cha mgonjwa kisha soma **Sura** au **Aya** za Quran zilizopohapa chini:

### 1. SURAT L-FAATIHA YOTE, (SURA INAYOANZA KATIKA QURAN TUKUFU)

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ (١)

﴿الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ (٢) الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ (٣) مَالِكُ يَوْمِ الدِّينِ (٤) إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ (٥) اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ (٦) صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ عَيْرَ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ (٧)﴾. سورة

الفاتحة

### 2. SURAT AL-IKH'LAAS YOTE, (SURA YA 113).

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ (١) اللَّهُ الصَّمَدُ (٢) لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُوَلَدْ (٣) وَلَمْ يَكُنْ لَّهُ كُفُواً أَحَدٌ (٤)﴾ سورة

### 3. SURAT AL-FALAQ YOTE , (SURA YA 114)

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ (١) مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ (٢) وَمِنْ شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ (٣) وَمِنْ شَرِّ النَّفَاثَاتِ فِي الْعُقَدِ (٤) وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ (٥)﴾ سورة الفلق

### 4. SURAT AN-NAAS YOTE, (SURA YA 115)

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ (١) مَلِكِ النَّاسِ (٢) إِلَهِ النَّاسِ (٣) مِنْ شَرِّ  
الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ (٤) الَّذِي يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ (٥) مِنَ الْجِنَّةِ  
وَالنَّاسِ (٦)﴾ سورة الناس.

## 5. AYAT AL-KUR'SI YOTE, (AYA YA 255) KATIKA SURAT AL-BAQARA

﴿اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُومُ لَا تَأْخُذُهُ سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ لَهُ مَا فِي  
السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عَنْهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ يَعْلَمُ مَا  
بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا حَلَفُهُمْ وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ وَسَعَ  
كُرْسِيُّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَا يَعُودُهُ حِفْظُهُمَا وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ  
(٢٥٥) لَا إِكْرَاهٌ فِي الدِّينِ قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ فَمَنْ يَكُفرُ  
بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِنُ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَى لَا انْفَصَامَ لَهَا وَاللَّهُ  
سَمِيعٌ عَلِيمٌ (٢٥٦)﴾ سورة البقرة.

## 6. AYA MBILI ZA MWISHO KATIKA SURAT AL-BAQARA, (AYA YA 285 – 286)

﴿أَمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلُّهُمْ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَا لَهُ كِتَابٌ  
وَكُتُبُهُ وَرُسُلُهُ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْ رُسُلِهِ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا عَفْرَانَكَ  
رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ (٢٨٥) لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا لَهَا مَا  
كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكتَسَبَتْ رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذْنَا إِنْ نَسِينَا أَوْ أَخْطَأْنَا رَبَّنَا  
وَلَا تَحْمِلْنَا إِصْرًا كَمَا حَمَلْنَا عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِنَا رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلْنَا مَا

لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِ وَاعْفُ عَنَّا وَاغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا أَنْتَ مَوْلَانَا فَانْصُرْنَا عَلَى  
الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ (٢٨٦). سورة البقرة

### Hili ni muhimu kueleweka

Inapaswa kufahamika kwamba, si lazima Sura hizo au Aya kuzifuatanisha hivyo bila kuanza na Dua nyingine. Katika Quran yote, hizo ndizo sehemu nilizoola ushahidi tofauti kutoka kwa Nabii (*swalla Llaaha alaihi wasallama*). Sura na Aya hizizina umhimu mkubwa.

### KUMSOMEA MGONJWA KIPANDE CHOCHOTE KATIKA QURAN

Inakubaliwa kumsomea mgonjwa kipande chote katika Quran. Katika kitabu changu '*Vinavyompasa Mwislamu kujua kabla hajasomewa Ruq'ya, (sehemu ya 1)*', nilithibitisha hadithi ya Mtume (*swalla Llaaha alaihi wasallama*) inayounga mkonomambo hayo.

Siku moja Mtume Muhammad (*swalla-Llahu alaihi wasallama*) alirudi kwake akamkuta mwana mke aliyekua anamtitibu mke wake Aisha (**RA**) akamwambia mwanamke huyo kwamba: '**Mtibu kwa Quran**'. Siku hiyo, Mtume Muhammad (*swalla Llaaha alaihi wasallama*) hakumbainisha mwana mke huyo **Sura** au **Aya** alizofaa kumsomea. Hii inaonyesha kwamba, Sura yoyote katika Quran ni *shifaa* (ponyo) *in-sha-Allah*.

Sababu nyingine ambayo inahakikisha hayo, Allah anasema katika Aya hii chini kwamba, Quran iliteremshwa kama tiba.

﴿وَنَزَّلَ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شَفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ وَلَا يَرِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا حَسَارًا﴾ . (سورة الإسراء: آية ٨٢).

"Na tunateremsha katika **Quran yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini**". Soma ( *Sura Bani Israil: Aya 82* ).

Katika Aya hiyo, Quran yote Allah aliitaja kama dawa, ikiwa na maana kwamba, sehemu yoyote unayoisoma katika Quran hua ni dawa.Lakini **Sura** ambazo nimetaja hapo nyuma na **Aya**, zina uzito. Mwislamu ambaye ana uzoefu wa kusomea wagonjwa **Ruq'ya**, anaweza kutoa ushahidi kwamba,sehemu hizo katika Quran humtatiza sana jini kuliko sehemu nyingine.

Kwa jinsi nyingine, nilionyesha katika kitabu hicho kwamba,kuna **Sura** au **Aya** nyingine ambazo wajuzi katika kusoma**Ruq'yawamezipendezesha** kusomwa.

Katika kitabu hicho nilieleza, na tena katika hiki nimerudia kwamba, ukiwa unamsomea mgonjwa sehemu hizo,kunakua na mabadiliko ya ajabu unayoyaona . Nyingine katika hizo Aya ndizo hizi hapa chini:

## 1. SURAT AL- A'ARAAF: AYA 106-122.

﴿قَالَ إِنْ كُنْتَ حِبْتَ بِآيَةً فَأَتِ إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ (١٠٦) فَأَلَّقَى عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ ثُعبَانٌ مُبِينٌ (١٠٧) وَنَزَعَ يَدُهُ فَإِذَا هِيَ بَيْضَاءُ لِلنَّاظِرِينَ (١٠٨) قَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمٍ فِرْعَوْنَ إِنَّ هَذَا لَسَاحِرٌ عَلِيمٌ (١٠٩) يُرِيدُ أَنْ يُخْرِجَكُمْ مِنْ أَرْضِكُمْ فَمَاذَا تَأْمُرُونَ (١١٠) قَالُوا أَرْجِهُ وَأَخْاهُ وَأَرْسِلْ فِي الْمَدَائِنِ حَاشِرِينَ (١١١) يَأْتُوكُ بِكُلِّ سَاحِرٍ عَلِيمٍ

(١١٢) وَجَاءَ السَّحْرَةُ فِرْعَوْنَ قَالُوا إِنَّ لَنَا لَأَجْرًا إِنْ كُنَّا نَحْنُ الْغَالِبِينَ  
 (١١٣) قَالَ نَعَمْ وَإِنَّكُمْ لَمِنَ الْمُقْرَرِينَ (١٤) قَالُوا يَامُوسَى إِمَّا أَنْ  
 تُلْقِي وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ نَحْنُ الْمُلْقِيْنَ (١٥) قَالَ أَلْقُوا فَلَمَّا أَلْقُوا سَحَرُوا  
 أَعْيُنَ النَّاسِ وَاسْتَرْهَبُوهُمْ وَجَاءُوا بِسُحْرٍ عَظِيمٍ (١٦) وَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِمْ  
 مُوسَى أَنَّ الَّقِيْقَ عَصَاكَ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِيْكُونَ (١٧) فَوَقَعَ الْحَقُّ  
 وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ (١٨) فَعَلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صَاغِرِينَ (١٩)  
 وَأَلْقَيْتَ السَّحَرَةَ سَاجِدِينَ (٢٠). سورة الأعراف

## 2. SURAT YNUS: AYA 79-82

﴿وَقَالَ فِرْعَوْنُ ائْتُونِي بِكُلِّ سَاحِرٍ عَلِيمٍ (٧٩) فَلَمَّا جَاءَ السَّحَرَةُ قَالَ  
 لَهُمْ مُوسَى أَلْقُوا مَا أَنْتُمْ مُلْقُونَ (٨٠) فَلَمَّا أَلْقُوا قَالَ مُوسَى مَا جِئْتُمْ بِهِ  
 السِّحْرُ إِنَّ اللَّهَ سَيْبُطِلُهُ إِنَّ اللَّهَ لَا يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ (٨١) وَيُحَقِّقُ  
 اللَّهُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ (٨٢)﴾ سورة يونس.

## 3. SURAT TWAHA: AYA 65-69

﴿قَالُوا يَامُوسَى إِمَّا أَنْ تُلْقِي وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ أَوَّلَ مَنْ أَلْقَى (٦٥) قَالَ بَلْ  
 أَلْقُوا فَإِذَا حِبَاهُمْ وَعَصِيْهُمْ يُحْيِلُ إِلَيْهِ مِنْ سِحْرِهِمْ أَنَّهَا تَسْعَى (٦٦) فَأَوْجَسَ  
 فِي نَفْسِهِ خِيفَةً مُوسَى (٦٧) قُلْنَا لَا تَخْفِي إِنَّكَ أَنْتَ الْأَعْلَى (٦٨) وَالَّقِيْقَ مَا  
 فِي يَمِينِكَ تَلْقَفُ مَا صَنَعْتَ إِنَّمَا صَنَعْتُكَ كَيْدُ سَاحِرٍ وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حِينَئِذٍ

﴿٦٩﴾ أَتَىٰ فَالْقِيَ السَّحَرَةُ سُجَّدًا قَالُوا آمَنَا بِرَبِّ هَارُونَ وَمُوسَىٰ (٧٠) سورة طه.

Aya hizo zilihakikishwa na wajuzi hawa hapa chini:

1. Shk.Abdullah Bin Baaz aliye kuwa Mufti wa Saudia katika kitabu chake'Al-Faawaa Al-Muta'alliqat bi-twibb).
2. Shk.Dr. Muhammad Bin Sulaiman, katika kitabu chake'Taf'siir al-Ush'r Al-Akhi'ir' Minal - Qur'aanil-Kariim).
3. Shk.Saeed Bin Ali Bin Walif al-Qah'twani, katika kitabu chake (Al-ILaaaji bi-Rruqaa Minal Kitaabi wa Sunnah).

Wajuzi hao wote watatu walikubaliana kwa sehemu hizo za Quran. Inaonekana Aya hizo zinausiwaa kwa sababu zinahusu mashindano baina ya wachawi wa Firauni na Nabii Musa AS.

Aya nyingine zinazousiwa, ndizo hizi hapa chini:

## 1. SURAT AL-BAQARA: AYA 1-5

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

﴿١﴾ إِنَّمَا (١) ذَلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ هُدًى لِلْمُتَّقِينَ (٢) الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِالْعِيْدِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمَمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ (٣) وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ إِمَّا أُنْزِلُ إِلَيْكَ وَمَا أُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ وَبِالْآخِرَةِ هُمْ يُوْقِنُونَ (٤) أُولَئِكَ عَلَىٰ هُدًىٰ مِنْ رَّبِّهِمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ (٥) ﴿٥﴾ سورة البقرة.

## 2. SURAT AL-KAAFIRUUNA YOTE

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

﴿قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ (١) لَا أَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ (٢) وَلَا أَنْتُمْ عَابِدُونَ مَا  
أَعْبُدُ (٣) وَلَا أَنَا عَابِدٌ مَا عَبَدْتُمْ (٤) وَلَا أَنْتُمْ عَابِدُونَ مَا أَعْبُدُ (٥)  
لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِيَ دِينِ (٦)﴾ سورة الكافرون

## 3. SURAT A'ALI IMRAN: AYA 18-19

﴿شَهَدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَاتِلًا بِالْقِسْطِ لَا إِلَهَ  
إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ (١٨) إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ وَمَا اخْتَلَفَ  
الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَعْيَانًا بَيْنَهُمْ وَمَنْ يَكُفِرُ  
بِآيَاتِ اللَّهِ فَإِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ (١٩)﴾ سورة آل عمران.

## 4. SURAT AL- A'ARAAF: AYA 29-32

﴿قُلْ أَمَرَ رَبِّيَ بِالْقِسْطِ وَأَقِيمُوا وُجُوهُكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَادْعُوهُ  
مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ كَمَا بَدَأْتُمْ تَعُودُونَ (٢٩) فَرِيقًا هَدَى وَفِرِيقًا حَقَّ  
عَلَيْهِمُ الضَّلَالُ لَئِنَّهُمْ أَنْهَمُوا الشَّيَاطِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ  
مُهْتَدُونَ (٣٠) يَا بَنِي آدَمَ حُذِّرُوا زِينَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَكُلُّوا وَاشْرُبُوا  
وَلَا تُسْرِفُوا إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ (٣١) قُلْ مَنْ حَرَمَ زِينَةَ اللَّهِ الَّتِي أَخْرَجَ  
لِعِبَادِهِ وَالطَّيَّاتِ مِنَ الرِّزْقِ قُلْ هِيَ لِلَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا حَالِصَةٌ  
يَوْمَ الْقِيَامَةِ كَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ (٣٢)﴾ سورة الأعراف.

## 5. SURAT AL -RAH'MAN: AYA 33-34

﴿يَا مَعْشَرَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ إِنْ أَسْتَطَعْتُمْ أَنْ تَنْفَدُوا مِنْ أَقْطَارِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ فَانْفَدُوا لَا تَنْفَدُونَ إِلَّا بِسُلْطَانٍ (٣٣) فَيَأْتِيَ آلَاءٌ رَّبِّكُمَا ثُكَّدِبَانِ (٣٤)﴾. سورة الجن.

## 6. SURAT AL-HASH'R: AYA 21-24

﴿لَوْ أَنَزَلْنَا هَذَا الْفُرْقَانَ عَلَى جَبَلٍ لَرَأَيْتَهُ حَاسِعًا مُتَصَدِّعًا مِنْ حَشْيَةِ اللَّهِ وَتِلْكَ الْأَمْثَالُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ (٢١) هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَالَمُ الْعَيْبِ وَالشَّهَادَةِ هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ (٢٢) هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْمَلِكُ الْفُطُوسُ السَّلَامُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَمِّمُ الْعَرِيزُ الْجَبَارُ الْمُتَكَبِّرُ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ (٢٣) هُوَ اللَّهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَى يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَهُوَ الْعَرِيزُ الْحَكِيمُ (٢٤)﴾ سورة الحشر.

## 7. SURAT AL -SSWAAFFAAT: AYA 1-10

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

﴿وَالصَّافَاتِ صَفَّا (١) فَالرَّاجِرَاتِ رَجَرًا (٢) فَالتَّالِيَاتِ ذِكْرًا (٣) إِنَّ إِلَهَكُمْ لَوَاحِدٌ (٤) رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَرَبُّ الْمَسَارِقِ (٥) إِنَّا زَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِزِينَةِ الْكَوَاكِبِ (٦) وَحْفَظَاهُ مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ مَارِدٍ (٧) لَا يَسْمَعُونَ إِلَى الْمَلَأِ الْأَعْلَى وَيُقْنَدُونَ مِنْ كُلِّ جَانِبٍ (٨)﴾

ثَاقِبٌ (١٠) سُورَةُ الصَّافَاتِ .  
دُخُورًا وَهُمْ عَذَابٌ وَاصِبٌ (٩) إِلَّا مَنْ حَطَفَ الْحَطْفَةَ فَأَتْبَعَهُ شَهَابٌ

## **8. SURAT AL-MU'UMINUUNA: AYA 115-118**

﴿أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا حَلَقْنَاكُمْ عَبَّاً وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ (١١٥) فَتَعَالَى  
اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ (١١٦) وَمَنْ يَدْعُ مَعَ  
اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الْكَافِرُونَ  
وَقُلْ رَبِّ اعْفُرْ وَارْحَمْ وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ (١١٨)﴾ سورة  
المؤمنون

## **9. SURAT AL-BAQARA: AYA 163-164**

﴿وَإِلَهُكُمْ إِلَهٌ وَاحِدٌ لَا إِلَهٌ إِلَّا هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ (١٦٣) إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاحْتِلَافٌ لِلَّيلِ وَالنَّهَارِ وَالْفُلْكِ الَّتِي تَجْرِي فِي الْبَحْرِ إِمَّا يَنْفَعُ النَّاسَ وَمَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنَ السَّمَاءِ مِنْ مَاءٍ فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ فِيهَا مِنْ كُلِّ ذَابِثٍ وَتَصْرِيفِ الرِّياحِ وَالسَّحَابِ الْمُسَحَّرِ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ (١٦٤)﴾ سورة البقرة.

## **10. SURAT AL-AH'QAAF:AYA 29-32**

وَإِذْ صَرَفْنَا إِلَيْكَ نَفَرًا مِنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ فَلَمَّا حَضَرُوهُ قَالُوا أَنْصِتُوا فَلَمَّا قُضِيَ وَلَوْا إِلَى قَوْمِهِمْ مُنْدِرِينَ (٢٩) قَالُوا يَا قَوْمَنَا إِنَّا سَمِعْنَا كِتَابًا أُنزَلَ مِنْ بَعْدِ مُوسَى مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ وَإِلَى

طَرِيقٍ مُسْتَقِيمٍ (٣٠) يَا قَوْمَنَا أَحِبُّوْدَا دَاعِيَ اللَّهِ وَآمِنُوا بِهِ يَعْفُرْ لَكُمْ مِنْ دُنْوِبِكُمْ وَجِرْكُمْ مِنْ عَذَابِ الْلَّيْمِ (٣١) وَمَنْ لَا يُحِبُّ دَاعِيَ اللَّهِ فَإِنَّهُ إِمْعَاجِزٌ فِي الْأَرْضِ وَلَيْسَ لَهُ مِنْ دُونِهِ أُولَيَاءُ أُولَئِكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ (٣٢) ﴿سورة الأحقاف﴾.

## 11. SURAT AL-JINN : AYA 1-9

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

﴿قُلْ أُوحِيَ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْتَمَعَ نَفْرٌ مِنَ الْجِنِّ فَقَالُوا إِنَّا سَمِعْنَا قُرْآنًا عَجَبًا (١) يَهْدِي إِلَى الرُّشْدِ فَآمَنَّا بِهِ وَلَنْ نُشْرِكَ بِرَبِّنَا أَحَدًا (٢) وَأَنَّهُ تَعَالَى جَدُّ رَبِّنَا مَا اتَّخَذَ صَاحِبَةً وَلَا وَلَدًا (٣) وَأَنَّهُ كَانَ يَقُولُ سَفِيهِنَا عَلَى اللَّهِ شَطَطًا (٤) وَأَنَّا ظَنَّنَا أَنْ لَنْ تَقُولَ الْإِنْسُونُ وَالْجِنُّ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا (٥) وَأَنَّهُ كَانَ رِجَالٌ مِنَ الْإِنْسِينِ يَعْدُونَ بِرِحَالٍ مِنَ الْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهْقًا (٦) وَأَنَّهُمْ ظَنُّوا كَمَا ظَنَّنْتُمْ أَنْ لَنْ يَبْعَثَ اللَّهُ أَحَدًا (٧) وَأَنَّا لَمَسْنَا السَّمَاءَ وَجَدْنَا هَا مُلِئَتْ حَرَسًا شَدِيدًا وَشُهِبًا (٨) وَأَنَّا كُنَّا نَقْعُدُ مِنْهَا مَقَاعِدًا لِلسَّمْعِ فَمَنْ يَسْتَمِعُ الْآنَ يَجِدُ لَهُ شِهَابًا رَصَدًا (٩)﴾. (سورة الجن).

## 12. Na Ayayoyote katika Qur'an inayozungumzia adhabu za moto.

Sehemu hizo zote ambazo nimezionyesha hapo juu, zilitayarishwa na Shk. Abdu-Salaam Waheed Baali katika kitabu chake 'Al-Wiqayaat, ukuraasa ya 72-75'.

## KUTUMIA AYA ZINAZOZUNGUMZIA 'UTULIVU' KATIKA KISOMO CYA RUQ'YA

Katika kuongezea juu ya Aya zilizopo hapo juu ambazo zimehimizwa na wazuoni wetu, kuna zile ambazo nitataja ndani ya mlango huu. Tutatazama Aya za Quran zinazohusiana na utulivu.

Katika kitabu chenye anwani '*Madaariju Al-Saalikiyna, 2/503*', muandishi Imam Ibn Al-Qayyim al-Jauzi 691-751HJ ambaye alikuwa mwanafunzi wa karibu sana wa Ibn Taymiyya 661-728 HJ, alisema:

"فَلَمَّا اشْتَدَّ عَلَيَّ الْأَمْرُ، قُلْتُ لِأَقْارِبِي وَمَنْ حُولَيْ: اقْرَأُوا عَلَيَّ آيَاتٍ السَّكِينَةَ، قَالَ: ثُمَّ أَقْلَعَ عَنِّي ذَلِكَ الْحَالُ، وَجَلَسْتُ وَمَا بِي قَلْبَةً". انظر "مدارج السالكين": ٢٥٣: لـ ابن القيم الجوزية.

"*Pindi mambo (ya mmaradhi) yangekua mazito kwa Sheikul-Islaam Ibn Taymiyya, angesoma Aya zinazohusu utulivu, na Allah swt alizitaja katila sehemu sita ndani ya kitabu chake (Qur'an)*".

Ibn al-Qayyim al-Jauzi...ambaye alikuwa mwanafunzi wa karibu sana na Ibn Taymiyya **661-728 HJ** alieleza katika kitabu chake hich hicho kuwa:

"*Wakati fulani kipindi Sheikh Ibn Taymiyya alisibiwa na ugonjwa na kuumwa kutokana na athari ya ugonjwa huo mkali, aliwaambia jamaa zake waliohudhuria kumsomea Aya za utulivu, na hali yake kiafia ikanawiri sana na akaketi kama yule ambaye alikuwa haungui kutokana na chochote....*".

Ibn al-Qayyim al-Jauzi691-751HJ alihitimisha kuwa, ye ye mwenyewe alijaribu kuzisoma Aya hizo zilizotajwa na akazipatakuwa zenye athari mno. Hivyo basi nawanasahi wenyewe kushugulika na kitendo hiki cha *Ruq'ya*, kuzisoma Aya hizi hapa chini zinazozungumzia utulivu:

#### 1. SUURAT AL-BAQARA: AYA 40

﴿وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ آيَةَ مُلْكِهِ أَنْ يَأْتِيَكُمُ التَّابُوتُ فِيهِ سَكِينَةٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَبِقِيمَةِ مِمَّا تَرَكَ ءَاءُلُ مُوسَى وَءَاءُلُ هَارُونَ تَحْمِلُهُ الْمَلَائِكَةُ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَا يَةً لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ﴾. (سُورَةُ الْبَقَرَةِ : آيَةُ ٤٠).

#### 2. SUURAT AL-TAUBA: AYA 26

﴿ثُمَّ أَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَنْزَلَ جُنُودًا لَّمْ تَرُوهَا وَعَذَابَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَذَلِكَ جَرَاءُ الْكَافِرِينَ﴾. (سُورَةُ التَّوْبَةِ : آيَةُ ٢٦).

#### 3. SUURAT AL-TAUBA: 40

﴿إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزِنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا، فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَّمْ تَرُوهَا وَجَعَلَ كُلَّمَا الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَى وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ﴾. (سُورَةُ التَّوْبَةِ : آيَةُ ٤٠).

#### 4. SUURAT AL-FAT'H: AYA 4

﴿هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ السَّكِينَةَ فِي قُلُوبِ الْمُؤْمِنِينَ لِيَرْدَادُوا إِيمَانًا مَعَ إِيمَانِهِمْ ، وَاللَّهُ جُنُودُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ عَلَيْهِمَا حَكِيمًا﴾ . (سورة الفتح : آية ٤).

## 5. SUURAT AL-FAT'H: AYA 18

﴿لَقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنْزَلَ السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَابَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا﴾ . (سورة الفتح : آية ١٨).

## 6. SUURAT AL-FAT'H 26

﴿إِذْ جَعَلَ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي قُلُوبِهِمُ الْحَمِيمَةَ الْجَاهِلِيَّةَ فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَلْزَمَهُمْ كَلِمَةَ التَّقْوَى وَكَانُوا أَحَقُّ بِهَا وَأَهْلَكُهَا وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلَيْهِمَا﴾ . (سورة الفتح : آية ٢٦).

**DUA UNAZOMSOMEA MGONJWA ALIYE SHIKWA NA MAJINI**

### DUA NO. 1

"بِسْمِ اللَّهِ يُبَرِّيئُكَ، وَمِنْ كُلِّ دَاءٍ يَشْفِيْكَ، وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ، وَشَرِّ كُلِّ ذِيْ عَيْنٍ". (رَوَاهُ مُسْلِمٌ).

"**BISMI-LLAHHI YUB'RIIKA, WA-MIN-KULLI DAAIN YASH'FIIKA, WA MIN SHARRI HAASIDIN". IZAA HASADA, WA SHARRI KULLI ZII AINI**". (Imesimuliwa na Imam Muslim).

"Mungu akuponye kwa jina lake, tena akuponye kila ugonjwa, akuponye ubaya wa mtu na husuda kama anakuwa amekuhusudu, tena akuponye kila ubaaya wa mtu na kijicho".

Dua hii, inapatikana katika '**Swahih Muslim**', na ilisimuliwa na bibi Aisha RA.

## DUA NO. 2

"بِسْمِ اللَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ أَعُوذُ بِاللَّهِ وَقُدْرَتِهِ مِنْ شَرِّ مَا أَجِدُ وَأَحَادِثُ<sup>٧</sup> (رَوَاهُ مُسْلِمٌ)

**"BIS'MILLA" X 3. "AUUZU BI- LLAAHI WA QUD'RATIHI, MIN SHARRIB MAA AJIDU WA U-HAAZIRU". X 7 .**

"Kwa jina la Allah (× 3). Nnajikinga kwa Allah na kwa uwezo Wake, aniponye na chokihisi(mwilini) na nachokihofia × 7".

Dua hiyo, inapatikana katika '**Swahih Muslim**', na ilisimuliwa na Uthman bin Affaan RA.

Dua hiyo, wewe mgonjwa ndiye unajisomea wewe mwenyewe. Kama haujui kusoma, unapaswa kusomewa na Shekhe.

## DUA NO. 3

"أَسْأَلُ اللَّهَ الْعَظِيمَ، رَبَّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ أَنْ يَشْفِيَكَ<sup>٧</sup>  
**"AS'ALU-LLAAHAL-AZWIIM, RABBAL-AR'SHIL-AZWIIM, AN-YASH'FIYAKA X 7".**

"*Namwomba Mwenyezi Mungu Mkuu, Mwenye arshi kubwa akuponye*".

Dua hii inapatikana katika '**Sunan Abu Dauda**', na ilisimuliwa na Ibn Abbas RA.

Dua hiyo, Mtume Muhammad (*swalla Llahu alaihi wasallama*) alisema hivi:

"*Yeyote anayemtembelea mgonjwa kabla hajaifikia ajali yake, akamsomea mara saba, mgonjwa huyo Allah atamponya ugonjwa huo*".

#### **DUA NO. 4**

"اللَّهُمَّ رَبَّ النَّاسِ، أَدْهِبِ الْبَأْسَ، وَاشْفِ أَنْتَ الشَّافِ لَا شِفَاءَ إِلَّا  
شِفَائُكَ، شِفَاءً لَا يُعَادِرُ سَقَمًا". (رواه البخاري)

**"ALLAAHUMMA RABBA-NNAASI, AZ'HIBIL-  
BA'ASA,WASH'FI ANTA SHAAFI, LAA SHIFAA-A  
ILLAA SHIFAA'UKA, SHIFAA'AN LAA YUGAADIRU  
SAQ'MAA".** Soma (*Swahih Bukhar*).

"*E Bwana Mlezi wa binadamu, ondoa ubaya wote, tena uponye, kwa sababu Wewe ndiye Mwenye kuponya, hakuna ponyo isipokuwa kuponya kwako, kuponya ambako ha kuachi ugonjwa*".

Dua hiyo inapatikana katika '**Swahih Bukhar**', na ilisimuliwa na Anas bin Malik R.a.

Siku moja Swahaba Anas bin Malik RA alimtembelea Thabit RA akiwa mgonjwa, akamwambia hivi:

"Ewe! Ni kutibu kwa matibabu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (Allah)? Akasema ndiyo! (akamsomea Dua hiyo)".

## DUA NO. 5

"بِسْمِ اللَّهِ الْأَرْقَيْكَ، مِنْ كُلِّ شَيْءٍ يُؤْذِنُكَ، وَمِنْ شَرِّ كُلِّ نَفْسٍ أَوْ عَيْنِ حَاسِدٍ، اللَّهُ يَشْفِيْكَ". (رَوَاهُ مُسْلِمٌ)

**"BIS'MILLAABI ARQ'IIKA, MIN-KULLI SHAY'IN YU'UZIika, WA MIN SHARRI KULLI NAF'SIN AU AINI HAASIDIN ALLAAAHU YASH'FIIKA".** Soma (Swahih Muslim).

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, nakutibu akuponye kinachokusumbua, na kila ubaya wa moyo au kila wa kijicho cha mtu wa husuda, Allah akuponye".

## DUA NO. 6

"أَعُوذُ بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَةِ، مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ وَهَامَةٍ، وَمِنْ كُلِّ عَيْنٍ لَامَةٍ". (رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ)

"Ninajikinga katika maneno ya Allah yaliyotimia, aniponye kila shetan, na kila mdudu wa sumu, na kila kijicho kinachoumiza". Dua hii, inapatikana katika '**Swahih al-Bukhar'**.

Dua hii, wewe mwenyewe mgonjwa ndiye mwenye kujisomea. Iwapo Sheikh ataamua kumsomea mgonjwa, neno la kwanza humo '**Authu**', linabadilika likawa '**Uithuka**'.

## DUA NO. 7

"أَعُوذُ بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَّاتِ مِنْ غَضَبِهِ وَعِقَابِهِ وَشَرِّ عِبَادِهِ، وَمِنْ هَمَزَاتِ الشَّيَاطِينِ وَأَنْ يَخْسُرُونَ". (رَوَاهُ التَّرمِذِيُّ).

*"A'UUZU BI-KALIMAATI-LLAHHI -TTAAMMAATI MIN-GADHABIHI WA IQAABIHI, WA SHARRI IBAADIHI, WA MIN HAMAZAATI-SHAY'TWAANI WA AN-YAH'DHURUUNI".*Soma (*Suna al-Tir'midhi*).

*"Najikinga katika maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyotimia, aniponye uchungu wake, adhabu zake, ubaya wa waja wake, kuwasiwishiwa ma Sheita'n na kunikaribia".*

Dua hio ilisimuliwa na Imam Tir'midhi katika kitabu chake '*Sunan Al-Tir'midhi*'.

Dua hiyo, anajisomea mugonjwa. Labda kama Shiek ameamua kumsomea mgonjwa, anabadilisha maneno mawili pekee; na ndio haya: Badala ya kusoma '*Authu*'-kwamba '*najikinga*', ansoma '*Uithuka*'-ina maana kwamba '*nakukinga*'. Lakini akiwa mgonjwa ni mwa mke, unasema '*U-iizuki*'.

Kingine unacho badilisha kwa Dua hio, ni neno la mwisho katika Dua hiyo linasomeka '*wa an yah'dhuruuni*'. Linabadilika na kuwa '*wa an yah'dhuruuka*'. Lakini akiwa mgonjwa ni mwana mke, inakuwa '*wa an yah'dhuruuki*'.

## DUA YA KUSOMEWA MAJINI WAKALI

Viumbe wa kijini kujifananisha na watu, kunazidiana nguvu na ujanja wa vita. Kuna jini ambaye anaweza kukusumbuwa ukashindwa kumtibu mgonjwa wako. Anaweza kuwa na nguvu nyingi, kama kukalia mkono wa mgonjwa ukawa kama nundu.

Jini kama huyu huweza hata kuwapiga watu makofi, mateke, kuuma, na wakati mwengine kupiga kelele. Anaweza hata kuzua uongo mfano wakiwa wamemtibu mwana mke, wanaweza kudai eti '***huyobwana amenibaka***', ama '***amenifanya hivi na vile***', kwa kumuabisha Sheikhe!

Wakati mwengine ukijaribu kusoma Quran, hupiga kelele kusudi asiweze kuisikia, vile vile kama unavyoona wanavyomkimbia anaadhini kwa shetani kutotaka kuisikia sauti ya adhana. Dua yenewe ni:

"أَعِيذُك بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَّاتِ الَّتِي لَا يُجَاهِدُهُنَّ بَرًّا وَلَا فَاجِرًّا، مِنْ شَرِّ مَا  
خَلَقَ وَبَرَأً وَدَرَأً، وَمِنْ شَرِّ مَا يَنْزِلُ مِنَ السَّمَاءِ، وَمِنْ شَرِّ مَا يَعْرُجُ فِيهَا ،  
وَمِنْ شَرِّ مَا ذَرَّا فِي الْأَرْضِ وَمِنْ شَرِّ مَا يَخْرُجُ مِنْهَا ، وَمِنْ شَرِّ فَتَنِ اللَّيْلِ  
وَالنَّهَارِ ، وَمِنْ شَرِّ كُلِّ طَارِقٍ إِلَّا طَارِقًا يَطْرُقُ بِخَيْرٍ يَا رَحْمَنْ". (رواہ الإمام  
أحمدُ فی مُسْنَدِه).

**"U-II'ZUKA BI-KALIMAATI-LLAABI-TTAAMMATI,  
ALLATII LAA YUJAAWIZUHUNNA BARRUN WA LAA  
FAAJIRUN, MIN SHARRI MAA KHALAQA WA BARA-  
A WA ZARA-A, WA MIN SHARRI MAA YAN'ZILU  
MINA-SSAMAA-I, WA MIN SHARRI MAA YA'ARUJU  
FIIHAA, WA MIN SHARRI MAA ZARA-A FIL-  
AR'DHWI, WA MIN SHARRI MAA YAH'RUJU  
MIN'HAA, WA MIN SHARRI FITANI- LLAY'LI WA-  
NNAHAARI, WA MIN SHARRI KULLI TWAARIQIN  
ILLAA TWAARIQAN YATW'RUQU BI HAY'RIN YAA  
RAH'MAAN"**

*"Nakukinga na maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyo kamilika, ambayo hayapiti mwema wala muovu, na shari ya alichokiumba, na akakitengeneza na kukianzilisha, na shari ya kinachoteremka kutoka mbinguni, na shari ya kinacho panda huko, na shari ya kinacho sambaa ardhini, na shari ya inayotoka ndani yake, na shari ya fitna za usiku na za mchana, na shari ya kila mtu anayegonga usiku, ila anayegonga kwa kheri, Ewe Mwingi wa rehma". Soma 'Mus'nad Al-Imam Ahmad, 3:119".*

‘Mgongaji’ anayesemwa hapo katika Dua, ni yule mtu anayegonga mlangoni kwako, au kwa mgonjwa kwa ubaya. Katika hawo wagongaji, kuna wazuri na wabaya. Hii Dua, unapomsomea mgonjwa wako, utakariri jinsi ilivyo, bila kubadilisha neno lolote.

Lakini utakapokuwa unajisomea, utabadilisha kwa neno la kwanza. Badala ya kusema ‘*U-ithuka*’, unasema ‘*A-uthu*’, Na akiwa mwana mke, badala ya kusema ‘*U- ihuka*’, unasema ‘*U-ithuki*’.

Dua hizo nilizozitaja, zinafaa kwa kila ugonjwa. Mwenye kushambuliwa na majini afaa kuzisoma au aliyepigwa kijicho, au ugonjwa mwengine wowote hata ikiwa homa au kidonda.

Dua zilizobaka zinapatikana katika kitabu cha Sheikh **Saeed bin Wah’fu al-Qah’twani** kina choitwa (*Al-Ilaaju Bi-Ruqaa*).

Ukisoma dua hizo ambazo nimezionyesha, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu majini wanakimbia haraka kwa mwili wa mgonjwa. Kwa sababu ya uwezo wa Dua hizo, majini

wanashindwa kuukimbia mwili, na huamua kumpanda mgonjwa kwenye ubongo wake.

Jini mshambulizi akiwa sio Mwislamu, utamwomba kusilimu. Allah akimjalia akasilimu, mwambie atafute majini wengine Waislamu akae nao.

Kuandamana naye, sio vizuri kwa sababu majini ni wadanganyifu sana. Jini anaweza kumwambia Shiekhe kwamba amesilimu kumbe anamdanganya akawa anaishi na shetani maisha yake yote. Masheikhe wetu wanafaa kukataza kitendo hiki, na kuwaonyesha Waislamu hatari ya kuishi na majini. Soma kitabu changu '*Yanayompasa Mwisilamu Kujua Kabla Hajasomewa Ruq'ya*'.

## TENDE NI DAWA DHIDI YA MAJINI

Mtende ni mti ambao una matunda yenyе baraka . Ndio maana Mwenyezi Mungu aliuweka katika Pepo (Jana). Mtu akishambuliwa na majini, anapaswa asubuhi kabla hajala chochote aanze kwa kula tende saba (7).

Mtume Muhammad (*swalla Llahu alaihi wasallama*) alisema hivi kuhusu tende:

"مَنْ اصْطَبَحَ بِسَبْعٍ تَرَاتٍ عَجُوْةً، لَمْ يَضُرُّهُ ذَلِكَ الْيَوْمُ سُمٌّ وَلَا شَجَرٌ".  
(مُتَّفَقُ عَلَيْهِ).

'Mtu akiamka asubuhi akala tende saba, siku hiyo hakuna uchawi au sumu ambayo itamdhuru'. Soma(Swahih Bukhar ).

Tende hizo zinafaa ziwe ni za mji wa Madina kama ilivyo kwenye Hadith sahihi. Soma (Swahih Bukhar 3: 168). Pamoja na hayo sina ushahidi wowote unaoonyesha

kwamba ni jinsi gani ya tende ndio muhimu, ama tende zenyе kupandwa katika mji wa Madina!

Lakini aliyekuwa Mufti wa Saudia, marehemu **Shk. Abdullah bin Bazi** alipendekeza kuwa, tende zozote zinaweza kuliwa kama dawa. Soma kitabu (*al-Ilaaj Bi-Ruqaa*) kilichoandikwa na Shk. Qah'twani.

## ASALI NI DAWA DHIDI YA MAJINI

Asali ni dawa, sio kwa mwenye kuvamiwa na majini pekee, lakini kwa kila ugonjwa mwingine. Allah aliyetukuka alisema katika Quran takatifu:

"يَخْرُجُ مِنْ بُطُونِهَا شَرَابٌ مُّخْتَلِفٌ أُولَئِنَّهُ فِيهِ شِفَاءٌ لِلنَّاسِ، إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ" (سُورَةُ النِّحْلِ: آيَةٌ ٦٩)

"Na kutoka matumbo yao (nyuki) kinatoka kinywaji chenye rangi mbali mbali; ndani yake kina MATIBABU kwa wanadamu. Hakika haya ipo ishara kwa watu wanaofikiri". Soma (*Surat An-Nah'l: Aya 69*).

Nyuki hufyonza mimea tofauti, kwa kuwa kwenye mimea watu hutoa dawa, ina maana kwamba ukinywa asali, unakua umekunywa dawa nyingi zenyе faida ya vitamini tofauti.

Mtume Muhammad (*swallah LLahu alaihi wasallama*) alisema :

"الشِّفَاءُ فِي ثَلَاثَةِ (وَذَكْرٌ مِنْهَا) شُرْبَةٌ عَسَلٌ" (رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ)

"Kutibiwa kupo kwa vitu vitatu, (kwa vitu hivyo vitatu kimo) kinywaji cha asali". Soma (*Swahih Bukhari*).

Kadhalika Mtume Muhammad (*swalla Llahu alaihi wasallama*) amesema katika Hadithi sahihi:

*"Ikiwa kuna kheri yoyote katika dawa zenu, basi ni katika hizi tatu: Kunywa asali, au kupiga chuku, au kuchomwa moto". Imesimuliwa na Bukhari na Muslim.*

Katika kitabu chake '**Al-Halaalu wal-Haraamu : 243**', ambacho kilifasiriwa katika lugha ya Kiswahili na bwana Salim Muhammad Elhaji, na kikachapishwa na **Wizara ya Wakfu na Mambo ya Kiislamu - (KUWAIT)**, mwandishi **Dr.Usuf al-Qaradhawi** alisema hivi kuhusu Hadithi hiyo :

*"Aina hizi tatu tukizichunguza tutaona kuwa, kulingana na dawa za kisasa zinazotumika, zinakusanya zile zakunywa, na zile zinazotumika katika utabibu waupasuaji, na zile zinazotumika katika utabibu wa spaki (umeme)".*

## **MAJI YA ‘ZAMZAM’ NAYO NI DAWA DHIDI YA MAJINI**

Kuna aina ya maji Allah ameweka baraka tena yana ponya ugonjwa. Maji hayo, Allah na Mtume wake Muhammad (*swallah Llahu alaihi wasallama*) ndio wanaostahili kutueleza, wala sio yejote kwa kauli yake mwenyewe. Kwa kuwa shetan anapenda sana kujifananisha na Mwenyezi Mungu, aliweza kueapoteza watu wengi kwa kuwambia kwamba, kuna maji fulani yanayoponya ugonjwa fulani.

Hapa Uganda, watu wengi wanatumia maji ya mto (*kitagata*) kwa ‘**kujitibu**’ ugonjwa wa aina nyingi, lakini huo ni upotovu dhahiri .

Kuhusiana na maji ya zamzam, Mtume Muhammad (*swalah Llahu alaihi wasallama* ) alisema hivi:

"..... إِنَّهَا شِفَاءٌ مُّسْتَدِّيٌّ . (رَوَاهُ الْبَرَّاُرُ فِي مُسْنَدِهِ) ."

"*Hakika (maji ya zamzam) ni dawa ya ugonjwa*". Soma *Mus'nad al-Bazzaar*.

Kwa kuwa Mtume Muhammad (*Swalla Llahu alaihi wasallama*) alisema ni dawa ya ugonjwa, inaonyesha wazi kwamba maji hayo yanaweza kumtibu mtu aliyeshikwa na majini.

Watu wengi wameyatuma nawakapata nafuu. Katika watu hao, ni tawapa mfano wa mtu mmoja, na ndiye Shk. Ibn al-Qayyim al-jauzi (691-796H. J). Katika kitabu chake kizuri '*Zaad Al-Ma'aad*', alisema hivi:

"وَقَدْ جَرِيَتْ أَنَا وَغَيْرِي مِنْ الْاسْتِشْفَاءِ بِمَاءِ زَمْزَمْ أُمُورًا عَجِيبَةً،  
وَاسْتَشْفَيْتُ بِهِ مِنْ عِدَّةِ أَمْرَاضٍ فَبَرِئْتُ بِإِذْنِ اللَّهِ" انظر (*رَأْدُ الْمَعَادِ*)."

"*Mimi mwenyewe na watu wengine, nilijaribu kujitibu kwa maji ya zamzam kwa ugonjwa mwingu, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nika pona*".

## ***HABBAT- SAUDA NI DAWA DHIDI YA MAJINI***

*Habbat -sauda* ni dawa inayojulikana sana. Huuzwa kwenye misikiti na kila sehemu zinapouzwa dawa za Kiislamu. Unaweza kuzitatua mbegu zake au kusaga na kuzichanganya na maji. Maji hayo (*solution*) utayasomea *Sura* na *Aya* za Quran takatifu ambazo nimeziorodhesha hapo nyuma.

Nabii (*swalah Llahu llaihi wasallama*) alisema katika Hadith sahihi kwamba:

"إِنَّ فِي الْحَبَّةِ السَّوْدَاءِ شِفَاءً مِنْ كُلِّ دَاءٍ إِلَّا السَّمْ." (مُتَّفَقُ عَلَيْهِ).

"*Hakika katika Habbat Sauda kuna dawa ya kila ugonjwa isipokua mauti (kifo)*". Soma (*Bukhar*) na (*Muslim*).

## MAFUTA YA ZAITUNI NI DAWA YA MAJINI

Mti huo haupatikani hapa Afrikca Mashariki, ila utaupata katika inchi za Uarabuni. Mafuta ya matunda ya mti huo, yanapikwa mboga, kadhalika watu wengine wanajipaka kama mafuta ya mwili.

Allah amesema katika Qurani takatifu:

"*Na mti utokao katika mlima wa Sinai, unatoa mafuta na kuwa kitoweo kwa walao*". Soma (*Surat Al- Mu'uminuuna* : Aya 20).

**Shk. Ali Muhsin Al-Barwani**, katika Tafsiri yake ya Kiswahili '*Tarjumat al-Mun'takhab*', alihakikisha kwamba mti huo katika Aya hii, ndio mzaituni. **Alisema hivi**:

"*Aya hii tukufu inathibitisha kuwa mti wa zaituni ni mionganini mwa miti alizo mneemeshea Mwenyezi Mungu binaadamu.....*".

Mti huo unaitwa '*olive tree*' kwa Kiingereza. Mtume Muhammad (*Swalla Llahu alaihi wasallama* ) amesema kuhusu mti huwo :

"*كُلُوا الرِّزْيَتْ، وَادْهِنُوا بِهِ، فَإِنَّهُ مِنْ شَجَرَةٍ مُبَارَكَةٍ*". (رواه الترمذى).

"*Mle mafuta ya mti wa zaituni tena mujipake mafuta yake, kwa sasabu mti huo una baraka*". Soma (*Sunan al-Tir'midhi*).

## **MKUNAZI (SID'RI) NI DAWA YA MAJINI**

Mti huu (*sid'ri*) kwa Kiswahili unaitwa *mkunazi*, na katika Kiingereza ukaitwa (*lote tree*). Mti huu majini hawaukaribii. Wajuzi wa Uislamu katika kusoma *Ru'qya*, ndio wamesema kwamba unatibu ugonjwa wa majini au uchawi. Mti huu, upo hapa duniani na pia huko mbiguni. Mti huo ni kama mtende au mzabibu.

Katika kitabu '*Fat'hul Haqqil Mubiin: 139*', mwandishi aliandika hivi kwa ufupi:

*"Twanga majani saba ya mti wa mkunazi (si'dri) yakiwa bado mabichi baina ya mawe mawili ama kitu chochote. Ukimaliza yaweke kwenye maji kiasi kinacho kutosha kuoga. Ni bora kuyasomea Aya za Ruq'ya. Utakunywa, kisha ya nayobaki utaumimiminia. Dawa hiyo ilijaribiwa kwa wagonjwa, na Mwenyezi Mungu akawaponya. Tena dawa hiyo ni nzuri sana hata kwa mtuambaye hawezi kumridhisha/kumtosheleza mke we".*

Dawa hiyo, Waislamu wanaosafiri katika nchi za Kiarabu, ni vyema kuitafuta na kuinunua, na mti huu sio ule '**sedero**' ya hapa Uganda.

Kwa kujengea hoja kwa dalili ya mti huo, nasema kuwa , kila mti unaojulikana kwamba unadhuru majini au uchawi, unapaswa kuchukuliwa kama dawa, kwa sababu nguvu hizo ambazo zinaponya, **Allah ndio amejalia**.

Hapa (Uganda) kuna mti unaitwa '**emmimbiri**' katika Lugha ya Kiganda. Mti huo ni sumu kwa sababu unawawua watu. Na hali kadhalika, kuna baadhi ya miti ambayo ni sumu kwa majini. Nawahusia Mashekhe wenzangu, ambao wana

shughulika na kazi yakusomea watu ***ruq'ya***, wajitahidi sana kutafuta miti ambayo inatibu uchawi au ugonjwa wowote.

Anayetaka kujua zaidi kuhusu miti hiyo, asome kitabu changu '***Yanayompasa Muislamu kujua hajasomewa Ruq'ya***'.

### **USAFI UNAFUKUZA MAJINI**

Katika kitabu '***Fat'hul Mu-iin***' ukurasa ya 142, mwandishi aliandika hivi kuhusu usafi:

*"Kuoga, kujiweka msafi na kujipaka marashi, ni moja wapo katika vitu vinavyofukuza majini".*

Hiyo sababu niya kweli sana, kwa sababu majini waharibifu wanapenda sana sehemu na mahala ambapo muna uchafu, tena Malaika wa Mwenyezi Mungu hawataki uchafu. Hii inamaanisha kwamba, mtu akiwa mchafu huwa amejifanya nyumba ya majini wabaya (***masheitani***), na Malaika ambao wangekusaidia kwa kufukuza majini washambulizi wanakutoroka.

### **KUJIKINGA KIJICHO**

Katika kitabu changu kinachoitwa '***Yanayompasa Muislamu kujua hajasomewa Ruq'ya***', nilionyesha ushahidi kutoka katika hadithi za Mtume Muhammad (*swalah Llahu Alaihu wasallama*) unaoonyesha kwamba kijicho kipo na kinashika na kudhuru watu-Mwenyezi Mungu akipenda.

Niliahidi katika kitabu hicho kuonyesha namna yakujikinga kijicho, kwa sababu '***kujikinga ni bora kuliko kujitibu***'.

Katika kitabu chake '*Badaa iu al-Fawaaid, 2/ 238-245*', Shk.Ibn Al-Qayyim-Al Jauzi (**691-756 H.J.**), alionyesha jinsi kumi anavyojikinga mtu na kujiepusha na kijicho, na aliandika hivi :

1. Kujilinda kwa Mwenyezi Mungu ili aweze kukulinda .(**Hii inamaanisha kumtii nakujiepusha kumuasi au kutenda aliyeyokataza**).
2. Kumtegemea Mwenyezi Mungu pekee, kwa sababu anayemtegemea, humfanyia mambo yake kuwa mepesi.
3. Kutomuogopa mtu huyo na kutomfikiria sana.
4. Kurejea kwa Mwenyezi Mungu kwa vitendo vyako vyema, na kutenda kila kitu kwa ajili yake pekee.
5. Kusuburi, kuvumilia na kumnyamazia mtu huyo ambaye anakuhusudu. Usimwogobe wala usiweke kwa roho yako yale akufanyiyayo.
6. Kutubu dhambi zako zote, kwa sababu mtenda dhambi Mwenyezi Mungu humkhidhili na humdalilisha.
7. Kutoa sadaka na kutendea watu wema, kwa sababu kwa njia hiyo huenda Mwenyezi Mungu akakuondolea ugonjwa huo wa kijicho.
8. Unapomjua anayekuhusudu, kaa naye kwa uzuri. Pamoja na kuwa hili jambo sio jepesi, lakini Mwenyezi Mungu atakusaidia dhidi ya ubaya na madhara ya mtu huyo.
9. Kumwomba Mwenyezi Mungu akukinge na husuda na watu wenye roho mbaya, sanasana kusoma '*Surat al -Falaq*' pamoja na '*Surat al- Naas*'.

## KUOGA MAJI YA MTU ALIYEKUPIGA KIJICHO NI DAWA

Mtu akikupiga kijicho ukamfahamu, huyu aliye kupaiga hua amrisha ashike ***udhu***, kisha yale maji aliyo yaba kisha uyaoge mwili. Hiyo ndivyo jinsi moja katika jinsi nyingi za kujitibu kijicho. Mtu ambaye amepigwa kijicho akifanya hivyo, Mwenyezi Mungu anamponya hatari ya kijicho na hawezi kudhuriwa, ***in -sha -Allah***.

Bibi Aisha (RA) mama ya Waumini amesema kwamba:

"كَانَ يُؤْمِنُ الْعَائِنُ فَيَتَوَضَّأُ، ثُمَّ يَغْتَسِلُ مِنْهُ الْعَيْنُ". (رَوَاهُ مُسْلِمٌ)

"Mtu alipokuwa anapiga mwenzake kijicho, alikuwa ana amrisha kushika ***udhu***, ili alie pigwa kijicho awoge katika maji hayo". Soma (*Sunan Abu Dauda*).

Mtume Muhammad (*swalla Llahu Alaihi wasallama*) alisema kwamba :

"الْعَيْنُ حَقٌّ، وَلَوْ كَانَ شَيْئٌ سَابِقُ الْقَدَرِ، لَسَبَقْتُهُ الْعَيْنُ، وَإِذَا اسْتَغْسِلْتُمْ فَاغْسِلُوا" (رَوَاهُ مُسْلِمٌ).

"Hakika kijicho kipo, na ikiwa kungelikuwepo kitu chochote kinachoweza kutangulia qadar ya Mwenyezi Mungu, kingelikuwa kijicho". Soma (*Swahih Muslim*)

Hadithi ambayo namalizia nayo kuhusu kuoga maji hayo, ni kisa cha Swahaba anaye itwa **Sah'1 bin Hanif (RA)**. Palikuwa bwana aliye kuwa anaitwa ***A'amir bin Rabii-ah*** aliye mpiga kijicho alipomwona anaoga. Swahaba huyo ali anguka chini akiwa hawezi hata kuongea. Mtume Muhammad (*swalah Llahu alaihi wasallama*) alipolie lewa hivi, alituma mara moja Swahaba mwengine amuite. Alipokuja, Mtume Muhammad (*swalah Llahu alaihi wasallama*) alimlaumu sana akamwambia:

"اعْتَسِلْ لَهُ". (رَوَاهُ النِّسَائِيُّ).

### **Maana yake:**

'(Nenda) uoge (kwenye maji)'. Soma (Tir'midhi).

Hadithi hiyo, inaonyesha kwamba, ukioga kwenye maji ya huyo aliyekupiga kijicho, moja kwa moja unapona **In-sha-Allah**.

Kuna watu wanaouliza namna ya kumjua mtu aliekupiga kijicho. Mtu ye yote anayetaka kujua na kuelewa zaidi mambo ya kijicho, na namna ya kumjuwa mtu aliekupiga kijicho, akisome kitabu changu '**Yanayompasa Mwislamu kujua kabla hajasomewa Ruq'ya**'.

Katika kitabu hicho nilionyesha kwa urefu matokeo na asili ya kijicho, na pia nikaonyesha kisa cha **A'amir bin Rabiah** aliyempiga kijicho Swahaba, **Sah'l Bin Hanif (RA)**.

## **DUA UNAZOSOMA KUJIKINGA KUTOKANA KIJICHO**

Mwanzo unafaa kufahamu kwamba, kusoma *Surat al-Falaq*, inahusiwa kwa sababu Aya ya mwisho inahusu kujikinga kwa Allah kutokana na ubaya wa hasidi anapohusudu, kwa sababu asili ya kijicho ni husda. Mtu hasidi ndiye hutamani kuondoa neema alizowapa Mwenyezi Mungu waja wake.

Katika '*Surat al-Falaq*' inayosomwa kutokana na kijicho, unafaa kuongeza dua zifuatazo:

### **DUA NO. 1**

"بِسْمِ اللَّهِ يُرْبِيْنِي، وَمِنْ كُلِّ دَاءٍ يَشْفِيْنِي، وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ، وَشَرِّ كُلِّ ذِيْ  
عَيْنٍ" (رَوَاهُ مُسْلِمُ)

**"BIS'MI LLAHI YUB'RIINII, WA MIN KULLI DAA-IN YASH'FIINII, WA MIN SHARRI HAASIDIN, WA SHARRI KULLI ZII AINI".**

"Mungu aniponye kwa jina lake, tena aniponye kila ugonjwa, aniponye ubaya wa mtu wa husuda kama anapokuwa amenihu sudu, tena aniponye kila ubaaya wa mtu na kijicho".

Dua hiyo, inapatikana katika '**Swahih Muslim**', ilisimuliwa na bibi Aisha RA.

## DUA NO. 2

"بِسْمِ اللَّهِ أَرْقِيْ نَفْسِيْ، مِنْ كُلِّ شَيْءٍ يُؤْذِنِيْ، وَمِنْ شَرِّ كُلِّ نَفْسٍ أَوْ  
عَيْنٍ حَاسِدٍ، اللَّهُ يَشْفِيْنِي". (رَوَاهُ مُسْلِمُ)

**"BIS'MI LLAHI AR'OH NAF'SII, MIN KULLI SHAY'IN YU'UZIINII, WA-MIN SHARRI KULLI NAF'SIN, AU-AININ HAASIDIN ALLAAHU YASHFIINII".**

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, najitibu aniponye kina chonisumbua, na kila ubaya wa moyo au kila kijicho cha mtu na husda, Allah aniponye" .

## DUA NO. 3

"أَعُوذُ بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَةِ، مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ وَهَامَةٍ، وَمِنْ كُلِّ عَيْنٍ لَمَّا  
(رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ)

"*A'uuzu Bi-kalimaati Llaahi Ttaamma, Min Kulli Shay'taanin Wa-Haammah Wa-Min Kulli Ay'nin Laamnah*". Soma(*Swahiih*

"*Ninajikinga katika maneno ya Allah yaliyotimia, aniponye kila shetan, na kila mdudu wa sumu, na kila kijicho kinachoniumiza*".

Dua hiyo, inapatikana katika '***Swahih Al-Bukhar***'.

Dua hiyo, utajisomea wewe mwenyewe mganjwa.Iwapo Sheikh atakuwa mwenye kumsomea mganjwa, neno la kwanza humo '***A-uuzu***', linabadilika likawa '***U-iizuka***'.Kwa ufupi hiyo ndiyo jinsi ya kujitibu kijicho na husda katika Uislamu.

Pamoja na kuwa Dua hizo unazitumia kujitibu mwenyewe, lakini pia unaweza kuzitumia kwa kutibu mtu mwingine, na unasoma hivi:

"بِسْمِ اللَّهِ يُبَرِّئُكَ، وَمِنْ كُلِّ دَاءٍ يَشْفِيكَ، وَمِنْ شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ،  
وَشَرِّ كُلِّ ذِيْ عَيْنٍ" (رَوَاهُ مُسْلِمٌ).

***"BIS'MI LLAABI YUB'RIKA, WA MIN KULLI DAA-IN YASH'FIIKA, WA MIN SHARRI HAASIDIN IZAA HASADA, WA SHARRI KULLI ZII AINI".***

"Mungu akuponye kwa jina lake, tena akuponye kila ugonjwa, akuponye ubaya wa mtu na husuda kama anakuwa

*amekuhusudu, tena akuponye kila ubaaya wa mtu na kijicho".*

Dua hiyo, inapatikana katika '*Swahih Muslim*', na ilisimuliwa na bibi Aisha RA.

"بِسْمِ اللَّهِ أَرْقِيْكَ، مِنْ كُلِّ شَيْءٍ يُؤْذِيْكَ، وَمِنْ شَرِّ كُلِّ نَفْسٍ أَوْ عَيْنٍ حَاسِدٍ، اللَّهُ يَشْفِيْكَ". (رواه مسلم).

**"BIS'MILLAHI ARQ'IIKA, MIN-KULLI SHAY'IN YU'UZIINKA, WA MIN SHARRI KULLI NAF'SIN AU AINI HAASIDIN ALLAAHU YASH'FIINKA".** Soma (*Swahih Muslim*).

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, nakutibu akuponye kinacchokusumbua, na kila ubaya wa moyo au kila kijicho cha mtu wa husuda, Allah akuponye".

"أَعِيْذُكَ بِكَلِمَاتِ اللَّهِ التَّامَةِ، مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ وَهَامَةٍ، وَمِنْ كُلِّ عَيْنٍ لَامَةٍ". (رواه البخاري)

**"U-IIZUKA BI-KALIMAATI LLAAHI-TTAAMMA, MIN KULLI SHAY'TWANIN WA HAAMMAH WA MIN KULLI AY'NIN LAAMMAH".** Soma (*Swahiih Bukhar*).

"Ninakukinga katika maneno ya Allah yaliyotimia, akuponye kila shet'an, na kila mdudu wa sumu, na kila kijicho kinachoumiza".

Dua hiyo, inapatikana katika '*Swahih Al-Bukhar*'.

## **DUA ZINAZOHUSU KUJITIBU UGONJWA WOWOTE**

Kuna Dua nyingine ambazo hazihusiani na kujitibu uchawi tu, bali pia lakini zikiwa zinatumiwa kutibu ugonjwa wa aina nyingine. Kwa kuwa kijicho pia ni ugonjwa, inakubaliwa kutumia dua hizo. Kwa mfano dua nambari **2, 3, 4** na **7** ambazo anasomewa mtu ambaye ameshikwa na majini. Hata hizo zilizopo hapo juu ambazo nilizozitaja kwamba zinatibu kijicho, unaweza kuzitumia kwa ugonjwa wowote.

Ukiwa unaelewa vizuri Kiarabu, utaona kuwa zinaweza kutumiwa kujitibu ugonjwa mwengine. Aidha, kuna Dua nyingine ambazo nimeacha, kama unazifahamu, hamna ubaya wowote kuzisoma. Ni lile lisemalwo kwamba mtu ambaye amekupiga kijicho unywe mkojo wake sio ukweli, kwa sababu hakuna kitu cha haramu ambacho kiliwekwa ndani yake dawa na Mwenyezi Mungu .

## **KWA NINI ALLAH WAKATI MWINGINE HAAJIBU DUA ZA WAJA WAKE?**

Katika Qura'n tukufu, na katika Hadithi za Mtume Muhammad (*swalla Llahu Alaihi wasallama*), Mwenyezi Mungu alituamrisha kumwomba. Kumwomba Mwenyezi Mungu ni kumhakikishia kwamba, ye ye yupo. Aidha kwa kumwomba tunakuwa tunamthibitishia kwamba katika vitu vyote, hakuna chenye nguvu nguvu na uwezo kumshinda. Aidha tunakuwa tumehakikisha kwamba anasikia kinachoendelea hapa aridhini na huko mbinguni. Kwa kuwafurahisha waja wake ambao wawemwomba, Mwenyezi Mungu huwajibu Dua zao.

Lakini kutokana na Nabii Muhammad (*swalla Llahu alaihi wasallama*), Mwenyezi Mungu aliyetukuka anawajibu waja wake kwa jinsi tatu:

1. Kuna kipindi anakujibu kwa haraka.
2. Kuna wakati unachomwomba akakikupa siku ya mwisho (*Akhera*).
3. Na kuna wakati Mwenyezi Mungu akaamua kuondoa shida nyingine ambayo haukumwoba. Hii ina maana kwamba, Allah alipo sema katika Qura'n tukufu:  
“**وَقَالَ رَبُّكُمْ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ** .....niombeni nitakuitikieni.....”. Soma (*Surat Gaafir*: Aya 60), alikuwa kwa maana ya kutujibu huko kwa aina tatu. Maswahaba wa Mtume Muhammad (*swalla Llahu alaihi wasallama*) waliposikia maneno hayo, yaliwazidisha nguvu kwa kumwomba Mwenyezi Mungu. Walimwambia Mtume Muhamad (*swalla Llahu alaiha wasallama*): ‘.....kama ndio hivyo, tunaenda kuzidi sana (kumwomba Allah)’. Soma *Sunan al-Tir'midhi*: 5/ 566). Pamoja na kuwa Allah alituahidi kutujibu pindi tumwombapo, hata hivyo, kuna kipindi hatujibu. Hii hutokea kutokana na sababu zifuatazo:

- ❖ Kumwomba Mwenyezi Mungu wakati huo huo unaomba wengine ambao siyo Yeye, ukawa unamshirikisha katika *ibaada* ya Dua.
- ❖ Kujombea mabaya, kama kumwomba Mwenyezi Mungu akuue kwa sababu ya shida inayokukumba.
- ❖ Kumwombea mwenzako ubaya wakati hana ubaya wowote amekufanyia, kwa sababu hata kama amekufanyia ubaya unafaa kumsamehe.

- ❖ Kuomba kitu ambacho ni haramu katika dini. Kwa mfano mtu kumwomba Mwenyezi Mungu awezeshe kutekeleza hila zako mbaya, mathalan kufanikiwa katika kuiba au kuzini.
- ❖ Kuomba ukisema , '*Allah ! nipe kitu fulani kama unapenda*'.
- ❖ Kumwomba Mwenyezi Mungu shingo upande ; ukiwa unasema, lakini kwa ukweli Allah atanijibu au hatanijibu??!
- ❖ Kuomba kama moyo wako na akili zako hazipo kwa hicho unachokiomba.
- ❖ Kuomba leo, kesho na kesho kutwa baadaye ukaacha, kwa sababu unaona haupati majibu.
- ❖ Kula, kunywa na kuвая vitu vya haramu.
- ❖ Kuomba ukiwa unataka upate unachokiomba mara moja.
- ❖ Kuomba kitu ambacho Mwenyezi Mungu amehukumu kuwa hawezi kukibadilisha.
- ❖ Kuomba ukiwa unaimba, au maombi ambayo yanatofautiana na maombi ya Kiisilamu.
- ❖ Kuomba ukiwa unapiga kelele kwa sauti ya juu kama unayemwomba hasisikii.
- ❖ Kuomba wakati unapiga miunzi na makofi, kwa sababu maombi ya namna hii ya **Manasara**, **Mayahudi** na **Washirikina**.

Hizo ndizo sababu Allah hukataa kukujibu Dua zako. Kwa hivyo, kama haukujibiwa, unafaa uangalie katika sababu hizo. Ukipata hakuna hata moja, basi jua kwamba Mwenyezi Mungu atakujibu katika sababu zile tatu Mtume Muhammad (*swallah Llaahu alaihi wasallama*) alizozungumizia katika Hadith.Kumbuka wakati huo, huwa unakuwa wakati ya majaribio ambao unafaa kuvumilia na kusubirishana.

## **HITIMISHO**

Kitabu changu kinachohusu kutibu uchawi na kijicho, husda pamoja na magonjwa mengine, nimekihitimisha hapa. Kwa uwezo wangu mdogo, nadhani nimejitahidi kufafanua kwa ufupi mambo mengi muhimu yanayohusu kujitibu uchawi, pamoja na kuorozhesha Dua zizosomwa kuhusiana na kadhia hiyo.

Kwa kutaka kufupisha kitabu hiki, nimeamua kuziacha Dua nyingine,mwenye kuzifahamu anafaa kuzisoma katika tiba.

Nawausia ndugu zangu Waislamu kuwa, msikubali kutibiwa na Wapiga ramli, Wagangawa jadi, Manasara, Mayahudi naWashirikina. Nawahakikishia kwamba Allah aliyetukuka atawajibu maombi yenu Dua ambazo nimeandika katika kitabu hiki.

Namwomba Mwenyezi Mungu, Mwenye uwezo mwingi, aliyeziinua mbingu bila ya nguzo tunazoziona, aliyeshika ardhi hii na milima isitutingishe, namwomba anisamehe madhambi yangu yote. Namuomba Mwenyezi Mungu ambaye hakuzaa wala hakuzaliwa, anewekee baraka katika kitabu hiki, akifanye **elimu** itakayonifaa baada ya kufa.

Namwomba Mwenyezi Mungu, amwitikie mja wake ambaye atatumia Dua ambazo nimeziweka katika kitabu hiki, na nyingine ambazo sikuzitaja. Namwomba Mwenyezi Mungu, anisamehe kwa chochote ambacho nimeteleza humu , kwa sababu utukufu ni wake pekee, Mwenye kufanya yaliyo nyooka. **AMIIINA**.

**Nuuuh Uthman Abu Najibah**

**5/11/2021**

## **KUHUSU MMWANDISHI**

- 1)** Mwandishi, Nuhu Uthman (Abu Najiibah) 'Kibuuka' alizaliwa mwaka 1965, katika kijiji cha Kanika, wilaya ya Kalungu.
- 2)** Wazazi wake ni marehemu, Sheikh Uthman Bashir 'Mukasa' na bibi Sarah Kyamummi.

## **ALIHUDHURIA SHULE ZIFUATAZO:**

- Kikukumbi Muslim Primary School, Kalungu District.
- Kabukunge Demonstration School, Kalungu District.
- Kabigi Islamic Institute, Bukomansimbi District.
- Qur'tubah Islamic Institute – (**Kuwait**).
- Imam Muhammad Bin Saudi University – (**UAE**).
- Hii sasa ni mhubiri huru anayepatikana Kampala (Uganda).